SUPA JACKPOT
TZS. 1,151,104,636
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Nipashe
Ijumaa Septemba 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581427
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Mwinyi** aongoza harambee kukusanya Dola bilioni 2 za BBT

UKURASA 8



**Uamuzi** kesi ya Mdee, wenzake mwezi ujao

UKURASA 5



**Marekani,** Norway zamwaga mabilioni mabadiliko tabianchi

UK. 4

# Mageuzi makubwa yaja kilimo Afrika

• **MARAIS** wakubaliana uwekezaji miundombinu na masoko, Samia aanika mikakati Tanzania ... *Endelea Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa amesimama na Rais wa Kenya, William Ruto (kulia), Rais wa Burundi, Évariste Ndayishimiye (wa pili kulia) na Rais wa Senegal, Macky Sall, pamoja na viongozi mbalimbali wakati wa wimbo wa Taifa wa Tanzania, Afrika Mashariki na ule wa Umoja wa Afrika ukiimbwa wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 11



Hili la kuchimba dawa linahitaji dawa

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 8, 2023 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nje, ndani kinachokwamisha Darajala Mto Mirongo kubaki tatizo sugu

## Inakosimama tafsiri ya Rais Dk. Samia, nafasi ya polisi nchini kubeba uchumi

Na Mwandishi Wetu

KATIKA wiki hii msamiati 'Dar inachemka kama bahari' imechukua nafasi yake. Kwanza kimataifa, kumekuwapo mkutano wa siku tatu ulioisha jana kujadili mustakabali wa chakula na biashara yake barani Afrika na hatima ya mlo barani Afrika sasa na siku zijazo.

Lingine, ni makamanda wa Jeshi la Polisi nchini nao wakakutana kwenye ukumbi wao, Oysterbay, Dar es Salaam safari hii wakijadili tija na majukumu yao.

Kwa namna ya pekee, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akawa mwenyeji kote, akianza na maafande, kisha akapaa na ndege hadi Nairobi Kenya, kujadili mazingira ngazi ya Afrika na dunia, ambako akapewa kipaza sauti kuwasilisha mada mwanana.

Siku ya pili tu, akawa amesharejea nyumbani kuwahi mjadala wa sekta yake kipenzi ya kilimo inayompa robo ya pato la taifa; theluthi mbili ya ajira ya watu; chakula kwa asilimia zote hadi ana ziada anataka kusitiri waliokosa nje kwa bei nafuu; bila kusahau utajiri wa malighafi kuwezesha viwanda nchini na nje.

Hapo kwenye chakula akawa mwenyeji wa hadhira zaidi ya watu 3,000, ila jana pia akawa na faragha na marais wenzake saba, wakikaa meza moja kujadili kilimo na chakula Afrika.

Hapo nako wakawepo majirani zake wa Afrika Mashariki ambao wapo mapema tu wakatua Dar es Salaam, kama vile jirani yake wa Burundi, Evarsite Ndayishimiye. Ama kweli 'kazi iendelee', Mama yuko kazini!

Akiwa Kurasini anaongea na maofisa wa Polisi, akawaasa kwa mambo kadhaa. Kwanza, akawakumbusha uaskari wao kubaki wakamavu mbali na vitambi, ujumbe ambao si mgeni.

Watangulizi wa awamu tofati nao walishawahi kuyadokeza, lakini mara zote unagusa wengi, vyombo vya habari navyo kama kioo cha jamii wakaiweka mbele kwenye taarifa zao kwa umma, ukiwa ujumbe mzito.

Pili, Mama akalikumbusha Jeshi la Polisi nafasi yake inavyoweza kuchangia mipango ya maendeleo taifa, ambayo kimsingi wakitekeleza vyema, wanakuwa tayari wameshachangia kwa nafasi yao, Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

POLISI VS UCHUMI

Huenda mtu anaweza kupata utata wa kinadharia na uhalisia katika uhusiano wa polisi na maendeleo ya moja kwa moja kiuchumi.

Ufafanuzi wa kina wa Rais Dk. Samia, mtaalamu wa utawala wa umma na uchumi jamii, katika mazungumzo yake na makamanda wa polisi unabeba ishara ya uhusiano huo unaotegemea mchango wao askari.

Polisi ni nyenzo ya usalama wa raia na mali zake, inayotumiwa na utawala rasmi wa nchi kupata utawala bora. Pia, utawala bora ni msingi wa kupatikana demokrasia katika umma, hata kuwezesha kuwapo serikali iliyofanikiwa kiutawala

TAFSIRI ILIKOGOTA

Katika nadharia ya sayansi ya siasa, inaonyesha utawala ambao ni wa kiserikali unaendeshwa na kusimamiwa na nyenzo ya kisiasa. Hapo ndipo panapoonekana vyama vya kisiasa kuunda serikali, kuongozwa na sera ambayo ni tafsiri na nyenzo ya 'tunaendaje kiuchumi na maendeleo'.

Wanazuoni wa sayansi ya siasa kama vile David Easton na Harold Laswell, walitafiti na kupatia maana au tafsiri ya siasa, ikigota katika maana ya watu au mtu anavyosimamia umma na rasilimali zake, ambao kimsingi ndio uchumi.

Wachumi nao wakatafsri maana ya fani yao, kwamba ni kutumia rasilimali chache zilizoko kukidhi mahitaji mengi na nyeti, jamii hiyo ilivyo nayo.

Katika kile ambacho Rais Dk. Samia alikuwa akinena kwa hadhira ya maafande wa polisi katika mkutano wao, alibeba ujumbe wa utawala wa kisiasa kukidhi mahitaji ya kiuchumi kwa Watanzania.

Mara zote, ili kuwezesha hayo maono, siasa inarejea kwenye msaada wa nguvu za kiuchumi kuiwezesha kwa kutumia miundombinu ya serikali ambayo polisi ni sehemu yake, inatumika kufanikisha malengo yake.

Hapo sera za kisiasa zinahitimisha dira za kiuchumi na kijamii zinazopaswa kutekelezwa na mamlaka husika serikalini, zinazosimamiwa na sheria, pia mamlaka za kisheria.

Chochote ambacho serikali inalenga kufanikisha, jukumu la watekelezaji wakuu linarejea kwa umma ambao ndio wazalishaji, pia walipa kodi wakuu, ikizingatiwa nguvu kuu ya kiuchumi ya serikali kujiendesha iko kwenye kodi inayozalisha hata bajeti ya polisi.

Hiyo ndio inayoangukia, mathalani kauli ya Rais Dk. Samia akihimiza jamii ya Kitanzania kuchukua hatua kutekeleza malengo ya kisera, serikali ikiwapa mazingira bora ya kunufaika, ambako katika usalama wa mali na watu, polisi anapatikana.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea taarifa ya jeshi la Polisi, kutoka kwa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Camillus Wambura, mara baada ya kuwasili kwenye Bwalo la Maofisa wa Polisi, Oysterbay, Dar es Salaam, wiki hii. PICHA; MTANDAO.

INAENDELEA UK.12

UKURASA WA 4

## KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

### KORTI YAKUBALI MAOMBI MANNE, SHAHIDI WA NANE KURUDI KIZIMBANI

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekubaliana na maombi manne ya Upande wa Jamhuri katika kesi ya mauaji ya dada wa marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', Aneth Msuya, ikiwamo shahidi wa nane ...

## Polisi wapiga 'stop' mikutano ya Tundu Lissu

UKURASA 3

# Majaliwa amtwisha mzigo Biteko kupaa bei mafuta

UKURASA 2



**MICHEZO** **SIMBA YAANIKA SIRI KURUNDIKA MAKIPA** UK.24

**MAONI** UK.6

# Mageuzi makubwa kilimo Afrika

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Tanzania imejizatiti kuingia katika masoko ya chakula ya kikanda, akieleza namna nchi ilivyojipanga kulisha Afrika kwa mazao ya mchele, mahindi na mboga.

Pia, amesema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inaimarisha miundombinu ya usafiri wa maji, reli na barabara pamoja na mawasiliano ya kidijitali katika kuyafikia masoko.

Aliyasema hayo jana alipohutubia Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) jijini Dar es Salaam. Alisema Tanzania ina fursa kusafirisha mazao hayo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), nchi nyingine za Afrika na dunia kwa ujumla.

Alisema ili kuchochea kilimo biashara Tanzania inatekeleza miradi ya kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kupitia nchi kavu barabara na reli, majini na angani.

"Jitihada hizo zote zinalenga kuharakisha na kurahisisha biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine za Afrika hususani kupitia Ukanda Huru wa Biashara Barani Afrika (FTA), na tayari tumeanza utekelezaji kwa baadhi ya bidhaa na nchi saba za Cameroon, Misri, Ghana, Kenya, Mauritius, Rwanda na Tunisia," alisema.

Rais Samia alisema ili kurahisisha upatikanaji fedha katika kilimo, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imeelekeza benki zingine kupunguza riba ya mikopo ya kilimo hadi kufikia asilimia tisa na wanaendelea na jitihada za kuwavutia wanawake na vijana kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi.

Pia alibainisha kuwa jitihada hizo zinaratibiwa chini ya programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) na utekelezaji wa programu ya viwanda katika kilimo.

Alisema ni matumaini yake katika mkutano huo watabuni mikakati kuhusu namna ya kushirikiana katika kushughulika na changamoto ya usalama wa chakula na lishe miongoni mwa nchi za Afrika, kufungua fursa za kilimo biashara na fedha kwa ajili ya kusaidia mifumo ya chakula katika ngazi za kitaifa.

"Kutokana na utajiri wa maliasili zilizopo barani Afrika na fursa zilizopo, bara hili lilipaswa litoe suluhisho kwa changamoto ya mifumo ya chakula duniani. Tumebarikiwa kuwa na asilimia 60 ya ardhi inayofaa kwa kilimo duniani, na vijana ambao ni nguvukazi kubwa.

"Tumebarikiwa maji katika mito na maziwa makubwa, madini yanayoweza kutupa fedha za kutosha kuwekeza kwenye kilimo endelevu. Pamoja na yote hayo Afrika tumebaki kuwa ni walalamikaji badala ya kutafuta suluhisho kuelekea njia itakayoleta mapinduzi ya uchumi wa kijani," alisema.

Rais Samia alibainisha kuwa zaidi ya Waafrika milioni 283 wanalala na njaa kila siku, wengine wanapata utapiamlo na magonjwa yanayohusiana na lishe. Pia wapo wanaofariki dunia kwa kukosa chakula. Ni aibu isiyokubalika.

Rais wa Burundi Evarist Ndayishimiye alihimiza wadau wa maendeleo hususani Benki ya Maendeleo Afrika kuongeza nguvu katika sekta za kilimo na mifugo kwa kutoa zana za kisasa kama matrekta na teknolojia.

Pia alitoa rai ya kuongeza thamani ya mazao kwa kusindika ili kuongeza ajira na kuepuka kuuza bidhaa ghafi huku akishauri viongozi wenzake kupunguza vikwazo vya kibiashara mipakani na ushuru ili sekta binafsi ifanye biashara kwa urahisi na kwa tija.

Rais wa Kenya, William Ruto, alimpongeza Rais Samia kwa kupunguza vikwazo mpakani na kutoa fursa kwa wafanyabiashara kupeleka mazao nchini mwake.

Alisema Tanzania iko kwenye nafasi ya kuzalisha chakula kingi kuliko Kenya kutokana na kupata mvua kwa wingi zaidi kuliko nchi hiyo.

"Kulikuwa na watu wakorofi na wazembe ambao walidhani mpaka ni wa kuzuia, wakasahau kwamba mpaka ni kivukio," alisema.

Mkutano wa AGRF ulianza Septemba 4 mwaka huu na unatarajiwa kuhitimishwa leo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

***Imeandaliwa na Maulid Mbaga, Restuta James, Renatha Msungu na Jenifer Gilla.**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKA KUU YA TANZANIA

KANDA YA DODOMA

SHAURI LA MADAI NA . 15/2022

ALLIANCE FINANCE COMPANY LIMITED. ..........MDAIWA.

KWA : SASN AUTO GARAGE COMPANY LIMITED POPOTE PALE ULIPO.

YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA RUFAA NA . 15/2022 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA**: Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Dodoma, Mbele ya **Mhe. Jaji F . R. Khalfan,** wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu **( 9.00)** kamili Asubuhi siku ya Alhamis Alhamis tarehe **12/09/2023.**

**HIVYO BASI:** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO ,** Hautafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba Shauri hii itashughulikiwa na Mahakama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA:** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe **25** Mwezi wa **Augosti , 2023**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

THE HIGH COURT

217590502





Rais Mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akizungumza katika Mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Majaliwa amtwisha mzigo Biteko kupaa bei mafuta

**Na Romana Mallya,** DODOMA

IKIWA ni siku saba tangu, Dk. Dotto Biteko ateuliwe kuwa Naibu Waziri Mkuu, moja ya kazi kubwa ambayo amekabidhiwa kuitafutia ufumbuzi ni kupanda kwa bei ya mafuta.

Miongoni mwa sababu ambazo zinachangia ni upatikanaji wa nishati hiyo na kusababisha bei kupaa kila mara ni vita kati ya Russia na Ukraine na sasa kuwapo kwa uhaba wa Dola.

Bei za sasa zilizotangazwa juzi na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa mfano, petroli lita moja kwa sasa inauzwa Sh. 3,213 na dizeli Sh. 3,259.

Majaliwa, wakati akijibu maswali ya papo kwa papo bungeni jijini hapa jana, alimwagiza Dk. Biteko kushughulikia suala hilo ndani ya siku saba.

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi, alisema mafuta ni muhimu kwa taifa kwa sababu ni sehemu ya ulinzi na usalama wa nchi.

Alisema miezi ya hivi karibuni kumekuwa na upatikanaji mafuta wa shida. Bei zimekuwa zikibadilika bila mpangilio.

"Lakini katika hali ya kushangaza ni kwamba, wiki moja au mbili kabla ya kutangazwa bei mpya za mafuta, kama utaratibu ulivyo kwamba kila Jumatano ya kwanza ya mwezi, bei zinatangazwa mafuta huwa hayapatikani lakini bei ikishatangazwa yanaanza kupatikana," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Shangazi alihoji ni mkakati gani wa serikali kuhakikisha taifa linakuwa na mafuta wakati wote na yanapatikana kwa bei ambayo Watanzania wanaweza kumudu.

Akijibu swali hilo, Majaliwa alisema: "Kwa kuwa ameshaanza hiyo kazi, niendelee kumwagiza Naibu Waziri Mkuu kushughulikia hili. Muhimu zaidi nishati yenyewe ipatikane nchini. Suala la bei tunajua zinabadilika wakati wote."

Ili kukabiliana na hali hiyo, alisema kuna jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali kupitia mifumo ya upatikanaji wa mafuta. Alisema wizara imekuwa ikifanya jitihada kuhakikisha nishati hiyo inapatikana bila matatizo.

"Hata Kamati ya Bunge ya Nishati imekaa mara kadhaa na wizara kuona mwenendo wa upatikanaji wa nishati hii kwa sababu, ina msaada mkubwa katika maeneo mengi ndiyo inasaidia kufanya shughuli za kiuchumi ziweze Kwenda," alisema.

Majaliwa alisema kutokana na mabadiliko ya uongozi yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni, Dk. Biteko amefanya vikao kadhaa ndani ya wizara na kukutana na wadau.

"Ni muhimu kuhusisha pia taasisi zote za mafuta ikiwamo EWURA, wanunuzi wa mafuta kwa mfumo wa pamoja, tutengeneze kikao kikubwa na wizara kadhaa zinazohusika mfano Wizara ya Fedha.

"Ofisi ya Uratibu ya Waziri Mkuu, mkae pamoja mwone namna ya upatikanaji wa mafuta. Suala la bei tutaanza kuangalia baadaye kwa sababu huwa zinabadilika kutegemeana na upatikanaji.

"Lakini tupanue wigo wa waagizaji wa mafuta ili tuwe na mafuta mengi nchini kwa usalama wa taifa letu. Kama hili litafanyika ndani ya wiki moja, tutakuwa tumepata majibu na tutawapa taarifa Watanzania lakini tutahakikisha mafuta yanapatikana na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu atashughulikia hili," alisema.

**KAULI YA SPIKA**

Wakati huohuo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema: "Jambo moja ninataka kulizungumza la serikali ni hili la mafuta na changamoto tunazozipitia. Nitumie fursa hii pamoja na kwamba nilishampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, hili jambo wameshaanza kulifanyia kazi.

"Pamoja na hayo, ninafikiri ni wakati mwafaka kabla ya kuweka mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja, tulikuwa na mfumo mwingine. Tuliziona changamoto zake na sasa tulipokwenda kwenye mfumo huu mpya pia una changamoto zake."

Spika alisema anafikiri ni wakati sasa kwa serikali kufanya tathmini maalum kwa ajili ya mfumo huo mpya wa uagizaji mafuta.

"Kwa sababu haiwezekani mafuta yawe yanakuwapo wiki mbili, wiki mbili nyingine lazima tuanze kutafuta halafu bei ikitangazwa tu mafuta yanaanza kuwapo. Kama huu mfumo unatupeleka kwenye changamoto nyingi zaidi kuliko ule wa kwanza, basi tuangalie namna ya kuboresha ule uliokuwapo zamani," alishauri.

Alisema kama pia uliopo una mianya imeachiwa, ikifanywa hiyo tathmini itawaelekeza wapi ili izibwe na kutofika mahali watakapoanza kuona foleni halafu ghafla zinaondoka bei zikishatangazwa.

HABARI KITAIFA




Wakazi wa kitongoji cha Sinoni Kusini, wilayani Monduli mkoani Arusha, wakigombania kuchota maji kwenye gari ya Mamlaka ya huduma ya maji safi juzi, kutokana na kukosekana kwa maji katika eneo hilo kwa miezi mitatu, baada ya pampu inayosukuma maji kuharibika. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Polisi yapiga 'stop' mikutano ya Lissu

**Elizabeth Zaya na Abeid Makarabo**
(SJMC)

JESHI la Polisi wilayani Ngorongoro limezuia mikutano ya hadhara ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, leo na kesho.

Kwa mujibu wa barua ya Septemba 6, mwaka huu, kutoka Jeshi la Polisi Ngorongoro kwa CHADEMA, mikutano hiyo ilipangwa kufanyika katika kata tatu zilizoko katika tarafa ya Loliondo na mengine ya kata tatu katika tarafa ya Ngorongoro.

Jana, katika ukurasa wake wa Twitter, Lissu aliweka barua ya jeshi hilo ya kumtaka kusitisha mikutano hiyo, huku akisema ratiba ya kufanya mikutano katika eneo hilo iko pale pale.

"Polisi wamekataza mikutano ya hadhara Ngorongoro. Juzi serikali ya Rais Samia imekataza wabunge wa Ulaya kutembelea eneo hilo. Wanaficha kitu gani licha ya jitihada za serikali? Sisi tutakuwa Ngorongoro kesho (leo)," aliandika Lissu kuhusiana na katazo hilo katika barua iliyotiwa saini na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Ngorongoro, Peter Lusesa.

Sehemu ya barua hiyo ilisomeka: "Yahusu kusitisha mikutano tarehe 08/09/2023 na 09//09 2023. Rejea somo tajwa hapo juu, pia yako KUMB: Na CDM/NGOR/V.1/01 ya tarehe 04/09/2023.

"Tunapenda kukufahamisha kuwa barua yako tajwa tumeipokea ikiwa na maudhui kufanya vikao vya ndani na mikutano ya hadhara maeneo ya kata tatu zilizoko tarafa ya Loliondo na kata tatu zilizopo tarafa ya Ngorongoro."

"Hata hivyo, Tarafa ya Ngorongoro ni eneo la Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro na kwamba kuingia na kutoka eneo hilo ni sharti kufuata taratibu zinazosimamia eneo hilo (kupata kibali kutoka Mamlaka Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro). Aidha, kwa upande wa tarafa ya Loliondo, kulingana na taarifa mbalimbali tulizo nazo, haziruhusu kufanya shughuli za kisiasa hasa mikutano ya hadhara.

"Kutokana na sababu hizo hapo juu, tunaelekeza kwamba usitishe mikutano hiyo kwa sasa hadi wakati mwingine ambao utakuwa mwafaka kwa ustawi wa amani na utulivu wa wilaya yetu.

Tunatanguliza shukrani kwa ushirikiano wako na nawasilisha kwa hatua zako."

Baada ya Lissu kuandika na kuweka wazi barua hiyo ya Jeshi la Polisi ya kuwataka kusitisha mikutano yao, baadhi ya wanaomfuatilia kwenye akaunti hiyo walitoa maoni tofauti, huku wakiwaomba wanaomshauri atii ombi hilo la Polisi huku wengine wakimuunga mkono kuendelea na ratiba ya mikutano yake.

# TMX yajivunia kuuza tani 135,000 za mazao

**Na Beatrice Shayo**

SOKO la Bidhaa Tanzania (TMX), limesema mpaka sasa limeuza tani 135,000 za mazao, ikiwamo ufuta, kahawa, mbaazi na choroko.

Kadhalika, kutokana na kuwapo kwa soko hilo kumesaidia Halmashauri za Mkoa wa Kagera kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 2.9 za ushuru ikiwa ni ongezeko la asilimia 100 kwa mwaka 2022.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMX, Godfrey Malekano, wakati wa mkutano wa waandishi wa habari na wahariri, kuhusu kazi zinazofanywa na taasisi hiyo.

Alisema TMX ni mfumo rasmi unaokutanisha wauzaji na wanunuzi kwa pamoja na kufanya biashara ya mikataba ya bidhaa, inayotoa uhakika wa ubora, ujazo na malipo.

Alisema soko hilo huleta wanunuzi wengi wa ndani na nje ya nchi ambao siyo lazima wafike kwenye soko la bidhaa au nchini kwa kuwa mauzo katika soko hufanyika kwa kutumia mfumo wa kidijitali ambao huwawezesha wanunuzi kufanya ununuzi popote walipo.

Aidha, alisema dira yao ni kuwa na soko linaloongoza, anuwai zaidi na linalokwenda na wakati katika nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

"Kutoa huduma za kisasa zenye ufanisi kwa uwazi na uadilifu kupitia jukwaa la kuaminika la mauzo ya bidhaa kwa njia ya teknolojia ya hali ya juu katika kutekeleza na kutimiza malengo ya maendeleo ya taifa," alisema.

Alisema masoko ya bidhaa yamekuwapo duniani na yana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi husika.

Aidha, alisema juhudi zilizofanyika mpaka sasa ni kwamba mfumo wa kieletroniki unaendelea kuboreshwa na kuongeza bidhaa zaidi kwa ajili ya mauzo.

Kwa mujibu wa Mlekano, TMX umesaidia kuongeza gharama kwa baadhi ya mazao kutoka Sh. 400 hadi Sh. 1,870 na wananchi kufaidika.

Alisema faida ya kuwapo kwa soko hilo ni kuimarisha bei ya soko zaidi ya Sh. bilioni 248.74 zimelipwa kwa wakulima, upatikanaji wa taarifa za soko, wakulima wapo huru kuamua bei walioridhia kuuza bidhaa zao, kuongezeka kwa ufahamu wa uzalishaji bora na uhakika wa malipo.

Aidha, alisema kumekuwa na changamoto ya uhifadhi wa mazao nyumbani kutokana na maghala kuwa machache.

Malekano alisema ipo haja ya serikali kuongeza maghala ya kuhifadhi chakula, ili waweze kufanya kazi kwa urahisi.

Aidha, alisema soko la bidhaa litaendelea kutoa elimu na kuwafikia wadau wengi zaidi, ili wafahamu mchango wao katika uchumi wa nchi. Alisema wataendelea kujiendesha kwa ufanisi, kidijitali na kutoa huduma zake kwa uadilifu ili kulinda maslahi ya washiriki wake wote. "Kazi ya kujenga mfumo imara wa Soko la Bidhaa inategemea na mchango wa serikali, taasisi na sekta binafsi, hivyo basi ushirikiano ni muhimu kufikia adhma hiyo," alifafanua.

Malekano alisema wataendelea kufanya utafiti kwa kushirikiana na wadau husika ili kuongeza bidhaa zaidi na wakulima kunufaika kupitia mazao yao.





Baadhi ya wakazi wa Kitongoji cha Kwa Kibosha, Mtaa wa Mpiji Darajani, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, wakikusanya mabaki ya vitu vyao baada ya kuvunjiwa nyumba zao na mtu anayedai kuwa amejenga kwenye eneo lake, ambapo nyumba 15 zilivunjwa jana na kuziacha familia zikikosa mahala pa kuishi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Korti yakubali maombi manne, shahidi wa nane kurudi kizimbani

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekubaliana na maombi manne ya Upande wa Jamhuri katika kesi ya mauaji ya dada wa marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', Aneth Msuya, ikiwamo shahidi wa nane kurudi tena kizimbani kuelezea kuhusu ripoti ya awali ya Jeshi la Polisi.

Uamuzi huo ulitolewa juzi na Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama hiyo baada ya pande mbili kuibua hoja zilizoibua mvutano.

Jaji Kakolaki alisema mahakama imealikwa na Upande wa Jamhuri kwa maombi manne - la kwanza ni kuachana na shahidi Jumanne Malangahe, kumwita tena Inspekta Fredrick Nyudike kuwasilisha taarifa halisi ya awali ya uhalifu.

Alisema jambo lingine ni kumwongeza shahidi Sajenti Obadiah aliyekuwa mtunza vielelezo na aliyepokea taarifa hiyo ofisini kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na kuruhusu ahirisho la kesi hadi Ijumaa (leo) ili kuleta mashahidi wengine kupitia maombi waliyoyafanya.

Alisema mahakama imepitia maelezo ya pande zote na kuyapa uzito na kupitia sheria zinazohusu maombi hayo, imekubali ombi la kwanza la upande wa mashtaka kuachana na shahidi kwa kuwa halikupingwa.

Katika ombi la pili, Jaji Kakolaki alisema kuwa baada ya kupitia kumbukumbu za mahakama, hakuna ubishi kwamba nakala ya taarifa hiyo ilitolewa na kupokewa kama kielelezo na shahidi namba nne ambaye alikataa kufahamu kilichomo na pia hakuulizwa lolote.

"Shahidi namba nane alipoitwa hakuulizwa swali lolote la dodoso kujua walichokuwa wanakitafuta upande wa utetezi hadi alipoitwa shahidi wa 22 na kuulizwa maswali ya dodoso.

"Ninakubaliana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Yasinta Peter, kuwa kifungu cha 147 hakikatazi kuita tena shahidi, lakini pia mahakama inaona kuwa upande wa utetezi utakuwa na nafasi ya kuuliza ili kujua walichotaka kukifahamu, hivyo pingamizi hili linakataliwa," alisema.

Jaji huyo pia alisema hakuna ubishi kama taarifa hiyo iko katika maandishi, imekidhi kigezo cha kwanza na kuna majina ya shahidi, kielelezo kitakacholetwa na maelezo ya ushahidi unaotakiwa kuletwa kama kifungu cha 289(4) CPA kinavyoeleza.

"Mahakama imechunguza taarifa hii, maelezo yaliyotolewa ambayo ni taarifa halisi ya awali ya tukio la uhalifu iliyotolewa kwa RCO Temeke na kwa DCI," alisema.

Kuhusu maelezo ya shahidi Obadia kwamba ndiye aliyepokea taarifa hiyo, na mtunza nyaraka na kumbukumbu ofisi ya DCI kuambatanisha kielelezo kwenye notisi, Jaji alisema si sharti la lazima, lakini kwa ajili ya haki, upande wa utetezi wapewe nakala hiyo mapema. Wajue maudhui yake na wajiandae mapema.

Hivyo, Jaji aliamuru upande wa mashtaka wawapatie upande wa utetezi nakala hiyo kufikia Septemba 7 mwaka huu (jana) na wasipofanya hivyo, hawatoruhusiwa kutumia ushahidi huo. Kuhusu hoja ya taarifa kutokutiwa saini, Jaji alisema mahakama imeona halina mashiko kwa kuwa ushahidi unaongozwa na nyaraka iliyowasilishwa mahakamani ambayo imekidhi matakwa ya kisheria.

Pia, alisema suala la kuahirishwa kesi kwa minajili ya haki, ni bora mahakama ikaruhusu ahirisho ili kuwapa nafasi kuandaa na kuleta mashahidi, hivyo kwa jana (Alhamisi) isingewezekana kuendelea na kesi hiyo.

Hivyo, mahakama iliruhusu ombi la ahirisho na kwa sababu hiyo, mahakama iliyakataa mapingamizi yote. Kesi itaendelea kusikilizwa leo Ijumaa na upande wa Jamhuri unapaswa kupeleka mashahidi na pande zote wapewe mwenendo wa kesi.

Kabla ya uamuzi huo wa mahakama, Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, alidai maombi ya kumwita shahidi huyo wanapinga kwa sababu alishakuja kutoa ushahidi akiwa na ripoti hiyo ambayo ni kielelezo.

"Wanataka kuleta yao ili kulinganisha, kwa sababu shahidi huyu ni wao na yeye ndiye alitoa hiyo ripoti na wao walikuwa wanajua alikuwa anakuja kutoa ushahidi, sioni sababu ya kumwita tena.

Na iko wazi kabisa ombi la kumwita kuja kuzungumza limetokana na maswali niliyomwuliza shahidi wao SSP Mhanaya. Kwahiyo, wanataka kuja kuziba mapengo ya shahidi huyu," alidai.

Wakili Kibatala alidai kuwa ni kweli kifungu cha 147(4) kinaruhusu hilo, lakini kinavyotumika haikukusudiwa hivyo kwa kurudiarudia mashahidi, vinginevyo kesi itakuwa haiishi.

"Tangu tuanze kikao hiki cha mahakama na kilichopita cha mwezi Juni, wana kazi ya kuongeza mashahidi wa ziada, mwanga wake ni nini kama kila siku kuomba? Walileta taarifa ya kumwongeza daktari ili aje kutoa ripoti ya uchunguzi wa mwili marehemu.

"Agosti 21, 2023, Dk. Chande kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikuja kutoa ripoti, Wiki mbili baadaye wanaongeza shahidi mwingine kuja kupambana na 'cross examination' na wanaomba kuongeza nyaraka," alidai Wakili Kibatala.

Aliendelea kudai: "Taarifa hiyo ni maneno yaleyale aliyoyadai SSP Mhanaya kuwa nyaraka hiyo ni nakala, lakini Mheshimiwa Jaji, kifungu hiki kilitungwa ili kufikia malengo haya?

"Sasa, kwa hali hii tutakwenda kweli? Sasa mahakama inatakiwa kuangalia ili isije ikatumika vibaya na pia taarifa yao haioneshi kama imepokelewa na karani. Kwa hali hii, mshtakiwa namba moja hajapewa taarifa."

Katika hoja ya tatu, Wakili Kibatala alidai haelewi kitu ambacho kinafanywa na upande wa Jamhuri, kwa kuwa taarifa walipewa juzi, lakini wanaambiwa wangepatiwa nakala juzi, huku kukiwa na ombi la ahirisho juzi hiyohiyo.

Wakili Kibatala akielezea hoja ya nne, alidai upande wa Jamhuri uligundua juzi usiku kuwa ushahidi unafanana.

"Tunapinga kuahirishwa kwa kesi hadi Ijumaa, kwa sababu hakuna siku hata moja upande wa utetezi tuliomba ruhusa. Kama mimi sipo, basi Nehemiah Nkoko atakuwapo. Tunaomba mahakama iwaamrishe waendelee na kesi na ikishindikana, basi tuendelee kesho (jana) kwa amri," alidai Wakili Kibatala.

Inadaiwa kuwa Aneth aliuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni mke wa marehemu Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela.

## Marekani, Norway zatoa bil 32/- kukabili tabianchi

**Na Emmaloveness Mkanula,** TUDARCo

MAREKANI na Norway zimetoa zaidi ya Sh. bil 32.4 kwa ajili ya kukabili mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Marekani nchini, katika kuendelea kudhibiti mabadiliko ya tabiachi, Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), limetoa ufadhili wa dola milioni 10 (sawa na Sh. Bil. 25) kwa ajili ya kulinda ikolojia muhimu na kupunguza gesi ukaa.

Naibu Kiongozi Mkuu wa USAID nchini, Isobel Coleman, alisema Marekani imetoa fedha hizo katika miradi miwili ili kuhimili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Tanzania.

Alisema dola milioni nane (sawa na Sh. bilioni 20) zitatumika kuwezesha usimamizi bora wa serikali na vijiji katika kusimamia maliasili za nchi na kulinda ikolojia muhimu.

Aidha, dola milioni mbili (sawa na Sh. bil 5) ni kwa ajili ya kuwezesha jamii za Pwani na wavuvi kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni mradi wa heshimu bahari unaofanywa na USAID.

"Ufadhili huo ni majumuisho ya dola milioni 34 (sawa na Sh. bilioni 85) zilizotolewa na serikali ya Marekani kusaidia Afrika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika kongamano la hali ya hewa la Afrika," ilibainisha taarifa hiyo.

Katika hatua nyingine, serikali ya Norway imetoa ufadhili wa Sh. bilioni 7.4 kwa Tanzania ili kuwezesha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na mazingira.

Akitia saini mkataba wa makubaliano ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi baina ya Tanzania na Norway, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Sulemani Jafo, alisema fedha hizo zitaleta manufaa kwa Watanzania.

"Ufadhili wa Sh. bil 7.5 uliofanywa na Norway unalenga kuiwezesha Tanzania kukabiliana na mabadiliko ya kimazingira hasa katika shughuli za kilimo, nishati, maji, afya, ardhi na makazi na miradi mingine mtambuka.

"Leo hii tumeingia makubaliano na kutia saini ili kujenga mikakati madhubuti itakayowezesha serikali za mitaa kuwa na uwezo wa kupanga, kubajeti, kusimamia na kuripoti maswala yote yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi," alibainisha Jafo.

Waziri Jafo alisema ufadhili huo utasaidia shughuli mbalimbali hususani mifumo ya upatikanaji wa maji ikiwa ni ujenzi wa visima, malambo na kilimo nyumba.

Awali Balozi wa Norway nchini, Tonne Tinnes, alisema nchi hiyo inathamini mchango wa kuwaleta pamoja washirika wa maendeleo, ili kusaidia kuchukua hatua katika mabadiliko ya tabianchi.

"Makubaliano haya kwa kushirikiana na shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF) yanalenga kujenga uwezo wa taasisi za serikali za mitaa (TAMISEMI) kukabiliana na mabadiliko hayo katika ngazi ya jamii," alisema Tinnes.

Vilevile wataiwezesha TAMISEMI kupanga mipango madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko hayo ikiwamo kutenga fedha ili kuwezesha mikakati hiyo.

Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo, Peter Malika, alisema ushirikiano huu ni muendelezo wa miradi ya uwekezaji inayoendelea mkoani Dodoma.

"Ufadhili huu ni mwendelezo wa miradi mbalimbali katika wilaya za Chamwino, Kondoa na Mpwapwa pia na nyingine zilizomo katika mkakati ni maeneo ya Bahi, Chemba na Kongwa ikiwa na jumla ya maeneo sita yenye uhitaji zaidi.

"Pia miradi hii inalenga katika nchi yote ya Tanzania na baada ya Dodoma tutatazamia Coastal Region 'mikoa ya Pwani' ikiwamo Tanga, Dar es Salaam, pwani na Mtwara" alisema.



Katibu wa Bodi ya Wadhamini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Baraza la Wazee wa chama hicho, Roderick Luterubeka (kulia), akizungumza na Mawakili wanaowakilisha chama, Ipilinga Panya (wa pili kulia) na Edson Kilatu, baada ya kusikiliza kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama wa wabunge 19 wa chama hicho katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Tarehe uamuzi kesi kina Mdee yapangwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam, Oktoba 24, 2023 inatarajia kupanga tarehe ya kutoa uamuzi wa shauri la kuvuliwa uanachama lililofunguliwa na wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Hatua hiyo inatokana na jopo la mawakili wa wabunge hao kufunga kesi kwa upande wao.

Tarehe hiyo ilipangwa jana na Jaji Cyprian Mkeha, wa mahakama hiyo baada ya mahakama kupanga tarehe ya pande zote mbili kuwasilisha mahakamani hapo majumuisho ya mwisho ya shauri hilo kuwa Oktoba 19, 2023.

"Nimewapa mwezi mzima pande zote muwe mmewasilisha majumuisho ya mwisho na pia Septemba 21, 2023, wote muwe mmepewa mwenendo wa kesi hii kwa ajili ya maandalizi ya majumuisho ya mwisho,"

"Tukutane hapa Oktoba 24, 2023 ili nije niwapangie tarehe ya uamuzi," alisema Jaji Mkeha.

Kabla ya Jaji Mkeha kupanga tarehe hizo, jopo la mawakili wa wabunge hao, linaloongozwa na Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge na Edson Kilatu, liliomba dakika 10 za kujadiliana kuhusu Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa CHADEMA, Mary Joakim ambae bado hawajamwuliza maswali ya dodoso kutokana na kiapo kinzani alichokiwasilisha mahakamani huko.

Waliporudi mahakamani, Wakili Panya alidai wamezunguza na mjibu maombi namba moja (CHADEMA), wamejaribu kupiga simu kuulizia hali ya mgonjwa Joakim, hali yake haijatengemaa na hawajui lini atakuwa vizuri.

"Ili haki itendeke, walitaka kumwuliza mjumbe huyo maswali ya dodoso kwake ambayo walikuwa wanatarajia kuyapata kutoka kwake, watayaleta kwa njia ya majumuisho ya mwisho. Tunaomba tupatiwe mwenendo wa shauri hili," alidai Wakili Panya.

Awali, Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini, Francis Mushi (80), wakati akiulizwa maswali ya ufafanuzi na Wakili wa CHADEMA, Hekima Mwasipo, alidai kiapo cha Freeman Mbowe na John Mnyika hakipo mahakamani kutokana na muundo wa chama chao.

Pia alidai kuwa taarifa zote za kwenye kiapo kinzani, alipata kutoka Ofisi ya Katibu Mkuu wa CHADEMA. Yeye ni Mjumbe wa Bodi.

Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, Halima Mdee, na wenzake 18 walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022, wakiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia, wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

# Bashe aona fursa mpya vijana wa BBT

**Renatha Msungu na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewataka vijana walioko katika programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT), kutumia fursa ya uwekezaji inayotolewa na wawekezaji kwa ajili ya kuinua sekta ya kilimo nchini.

Bashe alitoa rai hiyo jana wakati akimkaribisha Rais Samia Suluhu Hassan kuhutubia Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) linaloendelea jijini Dar es Salaam.

Waziri huyo alisema wanapaswa kufuta dhana iliyoonekana awali kuwa wanakiogopa kilimo kwa kuchangamkia fursa hizo ambazo serikali imeamua kuzitoa kwa vijana kupitia sekta ya kilimo.

"Ninaomba vijana mtumie fursa hiyo kujitokeza kwa wingi kujikita katika kilimo. Tunahitaji kuona mnajiajiri wenyewe kupitia kilimo na si kusubiri kuajiriwa," alisema Bashe.

Waziri huyo pia aliishukuru serikali kutokana na kutoa hamasa kubwa ikiwamo kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo.

Alisema ifike wakati sasa kila mmoja atambue kilimo ni uti wa mgongo ambapo ukifuata kanuni kutoka kwa wataalamu wa Kilimo, utachangia kwa kiasi kikubwa vijana na wakulima wengine kupiga hatua moja mbele kiuchumi.

Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, alisema katika kongamano hilo kuwa zaidi ya asilimia 90 ya mbolea nchini inaagizwa kutoka nje huku chini ya asilimia 10 ikitengenezwa ndani ya nchi.

Alisema mbolea nyingi hivi sasa inatoka Russia, ambako upatikanaji wake umekuwa na changamoto kutokana na vita inayoendelea huko.

Pinda alisema hali hiyo imesababisha bei ya mbolea kupanda huku bidhaa hiyo ikiadimika na kuhatarisha usalama wa chakula kwa baadhi ya nchi za Afrika.

Rais wa AGRA Afrika, Dk. Agness Kalebata, alisema asilimia 50 ya chakula kinacholiwa duniani kinazalishwa kwa kutumia mbolea.

Alisema matumizi ya mbolea yameendelea kuwa hafifu kutokana na upatikanaji wake kuwa mdogo na hivyo kusababisha uzalishaji mdogo wa mazao.

Katika hatua nyingine, Tanzania imeingia makubaliano na Serikali ya Uganda kushirikiana katika udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayovuka mipaka na yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama katika maeneo ya mipaka.

Utiaji saini ulifanyika jana kati ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega na mwenzake wa Uganda Bright Rwamirama, pembeni mwa Kongamano la Chakula Afrika (AGRF).

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, alisema mkataba huo utahusisha pia ushirikiano wa maendelezo ya miundombinu ya maji na malisho, teknolojia ya uzalishaji wa maziwa, dhana ya afya moja ambayo itahusisha na Wizara ya Afya na kuandaa mipango ya utafiti.

Waziri Ulega alisema Tanzania kuna mifugo mingi ikiwamo ng'ombe milioni 36, mbuzi milioni 26, kondoo milioni tisa, kuku wa kienyeji na kisasa milioni 97 na nguruwe milioni tatu.

Waziri wa Mifugo wa Uganda, Bright Rwamirama, alisema wanahitaji kushirikiana katika kulinda afya wa mifugo kwa kuwa wote wanahitaji kuzalisha bidhaa ikiwamo ya nyama iliyo bora.

"Mataifa kama China yanahitaji bidhaa kama vile nyama iliyo bora. Kama kuna ugonjwa Uganda, Tanzania hawawezi kuuza, vivyo hivyo Tanzania kukiwa na ugonjwa, Uganda hatuwezi kuuza. Kwahiyo, tukishirikiana wote, tutauza na kufaidika," alisema Rwamirama.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | TOMONI FARMS LIMITED | SHAMBA LENYE HATI YA MAUZIANO YA SERIKALI YA KIJIJI, EKARI 194 | FRANKLIN G. BAGALLA | KIJIJI CHA TOMONI-KIBITI RUFIJI | 26/09/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0714939933
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

*217590402*

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli za Mawaziri, Mchengerwa, Silaa zitekelezwe kwa vitendo

**MAWAZIRI** na Naibu Mawaziri walioteuliwa au kuhamishwa wizara, mapema wiki hii walianza rasmi kutekeleza majukumu yao mapya huku wakitoa kauli mbalimbali kuhusu utendaji kazi kwa watumishi wa wizara hizo. Miongoni mwa mawaziri hao ni Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Jerry Silaa wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Akizungumza na watumishi wa makao makuu ya TAMISEMI mjini Dodoma, Mchengerwa alibainisha kuwa asilimia 45 ya wakuu wa wilaya hawatimizi makujumu yao ipasavyo. Aliweka bayana kuwa viongozi hao wamekuwa wakifanya mambo binafsi ikiwamo kufanya ziara nyumbani kwao, kuandaa mazingira ya kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu ujao.

Waziri Mchengerwa alisema kutokana na tabia hiyo, wakuu hao wa wilaya wameshindwa kuwasimamia wakurugenzi wa halmashauri katika kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali. Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, aliwaagiza wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kuwafuatilia viongozi hao ambao ni wawakilishi wa Rais katika maeneo hayo.

Silaa kwa upande wake, alisema anatamani siku 100 za kwanza za uongozi wake katika Wizara ya Ardhi, zitumike kutatua na kumaliza migogoro ya ardhi ambayo imetamalaki katika maeneo mbalimbali. Kwa kiasi kikubwa migogoro hiyo inatokana na wakulima na wafugaji ambao wamekuwa wakigombea maeneo kwa ajili ya shughuli zao pamoja na wawekezaji na wananchi kutokana na watu hao kuingia katika sehemu mbalimbali kujipatia ardhi ili kuwekeza miradi yao.

Katika kuhakikisha azma hiyo inafanikiwa, aliwaagiza watumishi wa sekta ya ardhi katika mikoa na halmashauri zote kuliweka jambo hilo katika mipango yao ya utendaji kazi za kila siku na kigezo cha kuwapima katika utendaji kazi wao ni kwa kiasi gani wametatua migogoro ya ardhi. Sambamba na hilo, aliwaonya watendaji na viongozi wa ngazi mbalimbali ambao wamekuwa chanzo cha migogoro hiyo kuwa watakaobainika, hawatavumiliwa hata kidogo na watachukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria.


Waliyoyazungumza mawaziri hao kuhusu TAMISEMI na Ardhi si mambo mageni kwa kuwa yamekuwa yakiimbwa na kila waziri anayeteuliwa lakini watendaji wamekuwa na vichwa vigumu na masikio mazito. Mambo hayo yamekuwa sawa na hadithi za alfu lela ulela. Migogoro ya ardhi imekuwa ikizidi kushamiri kutokana na watendaji kuwa sehemu ya kuibua matatizo ambayo sasa yamekuwa sugu.

Pia utendaji legelege kwa wakuu wa wilaya na wakurugenzi ni sawa na wimbo uliokinai masikioni mwa Watanzania. Baadhi ya wakuu wa wilaya wamekuwa kiguu na njia wakifanya ziara majimboni kwa ajili ya kusaka ubunge.

Ushahidi wa hilo ni maeneo mbalimbali na kwa kiasi kikubwa ni ya vijijini ambako wananchi wanakabiliwa na kero mbalimbali ambazo hazitatuliwi kutokana na viongozi wengi kufanya mambo yao binafsi na kusahau dhamana waliyopewa. Serikali inapeleka mabilioni ya shilingi katika halmashauri kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama vile elimu, afya, barabara na maji lakini mingi haikamiliki kwa sababu ya kukosa usimamizi.

Kauli za mawaziri hao zitekelezwe kwa vitendo kwa kuhakikisha kila mwenye nafasi katika sehemu husika, anatimiza majukumu yake ipasavyo. Matokeo tarajiwa kutokana na kauli hizo ni watu kuwajibika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri pamoja na kutatua na kumaliza kero za wananchi ikiwamo migogoro ya ardhi ambayo sasa imekuwa sawa na donda ndugu. Jambo la msingi ni kwamba wananchi wanatamani kuona kauli hizo zinageuzwa kuwa vitendo na wale watakaofikiri kuwa ni kauli za kisiasa wachukuliwe hatua stahiki ili iwe fundisho kwa siku zijazo watu kutambua kwamba uongozi ni utumishi na si sehemu ya kujineemesha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Gifty Kenny

# Wazazi shughulikieni elimu ya mtoto namna hii, muwe makini na mila zenu

**UMUHIMU** wa wazazi katika kushughulikia suala la elimu kwa watoto, ni muhimu sana ili kuweza kuendeleza mfumo bora wa kielimu kwa watoto hao, kwani elimu hiyo ni ufunguo wa maisha kwao.

Lakini, kutokana na sababu au vikwazo kama tofauti za utamaduni katika jamii, zimeweza kuwafanya wazazi kutokufatilia maendeleo ya elimu ya watoto.

Utamaduni unawaathiri wazazi kwa njia nyingi linapokuja suala la kufuatilia elimu ya watoto wao. Kwa mfano, katika baadhi ya utamaduni, jukumu kuu la mzazi litawezakana kwakutoa mahitaji ya msingi ya kielimu kwa mtoto na kutazamwa kama jukumu la shule pekee.

Pia, imani za kitamaduni na maadili yanaweza kuathiri mtazamo wa wazazi kuelekea elimu na ufuatiliaji wake.

Kutokana na migogoro ya kifamilia inaathiri wazazi katika kufuatilia suala la elimu kwa watoto wao kwa sababu inaweza kusababisha mawasiliano mabaya, ukosefu wa ushirikiano, na kutokuwa na umoja katika kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto.

Migogoro inaweza kuchukua muda na nishati ya wazazi na kuwafanya washindwe kuzingatia kikamilifu mahitaji ya elimu ya watoto wao.

Pia, kutokana na changamoto za kiuchumi, inaathiri wazazi katika kufuatilia suala la elimu kwa watoto wao kwa njia kadhaa.

Wazazi wenye hali ngumu kimaisha, wanashindwa kuwanunulia watoto wao mahitaji ya shule kama vitabu, madaftari, kalamu na sare zao, au kugharamia masomo ya ziada, jambo linalochangia watoto hao kutopata elimu bora wanayostahili.

Ugumu wa kimaisha, pia unasababisha wazazi wengi kipato wanachopata kutumia kununulia chakula cha familia na mahitaji mengine, wakishindwa kununua mahitaji ya shule ya watoto wao, hivyo kupunguza muda na rasilimali wanazoweza kuzitumia kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao.

Niongeze hoja nyingine kwamba, kukosekana elimu kwa wazazi hao au misingi midogo na inawafanya kuwa wazembe wakiwa na ufuatiliaji hafifu wa suala nzima la taaluma kwa watoto zao, kwa sababu ya kukosa ujuzi na maarifa ya kutosha ya kuwasaidia watoto wao katika masomo hayo.

Hapo hapo penye misingi midogo ya kielimu, imeweza kusababisha hisia za kutokuwa na uwezo au kutojiamini kwa wazazi, nayo ikiathiri motisha yao ya kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto zao.

Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto kwa Shule na Vyuo vya Ualimu, unatamka wazazi wanahitajika kutoa mahitaji ya msingi kwa watoto.

Vilevile inaendana na haja yao kuonyesha upendo, kujali na kutoa msaada kwa mtoto, wakimshirikisha kufanya uamuzi wa familia, ili kusaidia elimu ya mtoto, kuwezesha vitendo vya kuhamasisha, kuzingatia na kumsikiliza mtoto, kuheshimu haki na hadhi ya mtoto, na kuhamasisha kujieleza kwa mtoto.

Wazazi wanatakiwa kujihusisha na masuala ya elimu kwa watoto zao, kwani Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inaeleza endapo wazazi watakuwa wakiwafatilia watoto wao katika suala la taaluma, itasaidia kuboresha mahudhurio mazuri, tabia nzuri na watoto kupata alama bora katika masomo darasani.

Pia, ni jambo litakalowasaidia watoto kuonyesha ujuzi bora walionao katika jamii kukabiliana vyema na shule na kuongezeka usalama wa wanafunzi,kutokana na wazazi kufatilia mienendo, hata kubaini changamoto watoto wanazokutana nazo masomoni, hata zikatatuliwa na walezi, pia shuleni.

Vilevile walimu wana nafasi ya kushauriwa kujenga urafiki wa karibu kimasomo na wanafunzi wao. Ni hali inayowasaidia watoto kutowaogopa na kuwaeleza changamoto wanazozipata katika masomo. Nayo ni njia inayowaongoza watoto kuyapenda masomo, hatimaye wakafaulu vizuri.




Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Goodluck Urassa akizungumza wakati akiwajengea uwezo walimu wa shule za Kimataifa za St Mary's, jijini Dar es Salaam jana, ili waweze kuongeza ubunifu na ufanisi katika ufanyaji kazi wao. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbunge kupeleka muswada bungeni kuondolewa mamlaka ma-RC na ma-DC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, ameitaka serikali kupeleka muswada bungeni ili kuwaondolea mamlaka wakuu wa mikoa na wilaya ya kuwaweka watu ndani kwa saa 24 kutokana na kutumika bila kufuata taratibu.

Akiuliza maswali bungeni jana, Mbunge huyo alisema ripoti ya tume ya haki jinai iliyotolewa hivi karibuni imezungumzia matumizi mabaya ya waliopewa mamlaka Wakuu wa Mikoa na Wilaya namna wanavyotumia saa 24 kuwaweka watu ndani bila kufuata taratibu.

"Lini serikali italeta muswada ili kuwaondolea haya mamlaka na kubaki na jukumu la kusimamia maendeleo na jukumu hilo libaki kwa jeshi la polisi peke yake," alihoji.

Alisema semina elekezi ni muhimu baada ya kuteuliwa kwao.

Aidha, alihoji mpango wa serikali wa kutoa semina elekezi mara kwa mara kwa wakuu hao kuhusu utawala bora.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema tayari serikali imeshatoa taarifa ya kijinai na imeanza kufanyiwa kazi na wananchi wanashirikishwa kwenye maeneo mbalimbali ili kutoa maoni yao. "Baada ya maoni hayo taratibu zingine ikiwamo mabadiliko ya sheria ziweze kufuatwa, naomba wabunge na Bunge muwe na subira wakati mchakato wa kukusanya maoni ya watu unaendelea kufanyika na itakapokuwa tayari tuweze kuleta kama kutakuwa na mapendekezo ya sheria au miongozo yoyote ile sisi kama serikali tuweze kufanyia kazi," alisema.

Aidha, alisema serikali imeendelea kutoa semina elekezi kwa viongozi waliteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali ili kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sera, sheria na kanuni zilizopo.

"Kwa kipindi cha mwezi Februari hadi Agosti, mwaka huu serikali ilitoa mafunzo elekezi ambayo moja ya ajenda ilikuwa ni utawala bora," alisema.

# Hatimiliki 50,000 kutolewa kwa wakazi wa Chalinze

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

HATIMILIKI 50,000 zinatarajiwa kutolewa kwa wakazi wa kata za Halmashauri ya Chalinze zilizopo kwenye mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Miliki za Ardhi unaotekelezwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Hadi sasa vipande vya ardhi 7,615 katika Kata za Pera na Bwilingu, vimetambuliwa katika utekelezaji wa mradi huo.

Hayo yamebainishwa jana mjini hapa kwenye kikao cha wadau kujadili Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Miliki za Ardhi na Meneja wa mradi huo, Leon Mwenda.

Mwenda alisema mradi huo kwa hapa nchini utatekelezwa katika halmashauri 34 na kwamba zaidi ya Shilingi bilioni tatu zitatumika na hati 500,000 zitatolewa katika vijiji 250.

Alisema kwamba kikao hicho katika Halmashauri ya Chalinze kimelenga kupata ushauri wa namna ya kutekeleza mradi huo kwenye maeneo yaliyolengwa.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, akizungumza katika kikao hicho alisema mradi huo utasaidia kutokana na kuwapo na migogoro mingi ya ardhi.

Okash alisema kupitia mradi huo wananchi watanufaika kwa kupata hatimiliki za ardhi zao na pia wakazi watatambulika kwa urahisi na maeneo yao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhani Possi, alimshukuru Rais kwa kuwapo kwa mradi huo ambao utatekelezwa katika kata tisa na kwamba vipande 30 vitatambuliwa kwenye mradi huo.

Kata zilizopo kwenye mradi ni pamoja na Vigwaza, Pera, Bwilingu, Ubena, Msata, Kibindu na Miono.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



MKUTANO MFUKO WA CHAKULA AFRIKA

# CPB yaita wawekezaji maeneo matano

**Na Restuta James**

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), imeita wabia na wawekezaji katika maeneo matano ya fedha, teknolojia, wakusanyaji wa mazao toka kwa wakulima, usambazaji wa bidhaa na wakulima wakubwa na wadogo.

Akizungumza na wadau kwenye hafla ya kibiashara pembezoni mwa kongamano la Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) linaloendelea jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, David Silinde, alisema bodi hiyo inakusudia kutafsiri kwa vitendo malengo ya jukwaa hilo kwa kujumuisha vijana na wanawake katika uzalishaji wa mazao ya chakula.

"Bodi imejiandaa kukuza sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko ambayo ni muhimu katika mifumo ya chakula na kuchangia kapu la chakula la taifa," alisema.

Silinde alisema hafla hiyo inalenga kuchochea ushirikiano wa kibiashara na kampuni zinazoagiza nafaka kutoka Tanzania ili kuwa na mifumo endelevu ya chakula.

Awali, Mwenyekiti wa CPB, Salum Awadh Hagan, alisema bodi inahitaji wabia wenye mitaji ya fedha, teknolojia, usambazaji wa bidhaa na wakulima wakubwa.

Alisema mwelekeo wa bodi ni kujiendesha kibiashara ili kuwahakikishia wakulima soko la mazao yao.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa CPB, Gungu Mibavu, alisema wanahitaji mawakala wa kusambaza na kuuza bidhaa zao nchini na kukusanya mazao kutoka kwa wakulima, kwa kuwa waliopo hawatoshi.

"Mazao ambayo tunashughulika nayo kwa sasa ni mahindi, mpunga, ngano pamoja na alizeti pamoja na mbaazi," alisema.

Alisema wamepata mbia wa kuingiza kiasi cha ngano tani 15,000 na kwamba dhamira ya bodi ni kushirikiana na kampuni hiyo kuingiza tani 25,000 za zao hilo.

Kadhalika, alisema bodi ina mikataba ya kibiashara ya kuuza mahindi katika nchi za Rwanda na Burundi, ambayo wanayanunua kwa wakulima nchini.



Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhi cheti kwa mshindi wa GoGettaz, Hasina Andriatsitohaina kutoka nchi ya Madagascar, baada ya mdahalo wa vijana na kilimo, wakati wa mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Rais na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Yara International, Svein Tore Holsether (wa pili kulia) na (kulia) ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Mwinyi aongoza harambee ya kukusanya Dola bil 2 za BBT

**Na Jenifer Gilla**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Husein Ali Mwinyi, ameongoza harambee ya kuhamasisha washirika kusaidia Dola za Marekani bilioni mbili za utekelezaji wa mradi wa Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) wenye lengo la kuwezesha vijana kushiriki shughuli za kiuchumi kupitia kilimo, ufugaji na uvuvi.

Wadau mbalimbali wamehudhuria na kuahidi kuunga mkono mkakati huo ikiwamo Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) iliyoahidi kutoa Dola milioni 100 na Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani barani Afrika (AGRA) iliyoahidi Dola milioni 40, msaada kutoka Mifuko ya Bill and Melinda Gates and Matercard.

Akizungumza katika harambee hiyo iliyofanyika katika Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) jijini Dar es Salaam, Rais Dk. Mwinyi, alisema mbali na kupongeza ongezeko vijana na wanawake katika shughuli za kiuchumi Afrika, alisema ushiriki wao bado ni mdogo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na upatikanaji mdogo wa rasilimali za uzalishaji.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni ujuzi mdogo wa ujasiriamali katika kilimo, vizuizi katika mgawanyo wa rasilimali, ugumu wa upatikanaji wa mitaji katika kuendeleza ujasiriamali wao, upatikanaji masoko na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema ili kuhakikisha kuwa ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo na uvuvi unaongezeka na kuchangia kukua uchumi wa taifa, serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, wameandaa mikakati shirikishi na kutekeleza mipango mbalimbali kusaidia vijana na wanawake kujishughulisha na kilimobiashara kupitia mradi wa BBT.

"Vijana wana hamu ya kuwekeza pale ambapo wataweza kupata faida ya haraka katika sekta ya kilimo na uvuvi. Hili tumeliona kwetu Zanzibar kufuatia mipango tuliyoiweka ya utekelezaji wa miradi ya Uchumi wa Bluu katika jamii za mwambao wa Pwani kutokana na msaada wa fedha za ahueni ya UVIKO-19," alisema Rais Dk. Mwinyi.

Alisema vijana na wanawake wakiwezeshwa, watafungua milango zaidi ya ajira katika maeneo ya uzalishaji wa chakula, uongezaji thamani na masoko ya mazao ya kilimo na uvuvi na kujihakikishia uhakika wa chakula, lishe na kuondoa umaskini.

Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, alisema lengo la serikali ni kukusanya Dola bilioni kwa miaka sita kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa BBT unaoisha mwaka 2030.

Alisema hatua hiyo itawezesha ukuaji wa uchumi kwa kuwa kilimo kinachangia asilimi 25 ya Pato la Taifa huku asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo, kinatoa asilimia 75 ya ajira na kuchangia mauzo ya nje ya nchi kwa asilimia 85.

"Lengo la mradi wa BBT ni kujumuisha vijana zaidi ya milioni 16 katika mfumo rasmi wa kiuchumi kupitia kilimo kwa kuwapa elimu na uwezeshaji ambao kwa muda mrefu uliwaweka pembeni kutokana na kukosa elimu," alibainisha Bashe.

Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle, alisema nchi yake itaendelea kuunga mkono Tanzania kuboresha mifumo ya kilimo na mazingira ikiwamo uhifadhi wa matumbawe Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya Uchumi wa Bluu.

Alisema kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) na taasisi za maendeleo ya kama Bill and Melinda Gates, wanashiriki katika kukuza uchumi wa Tanzania kupitia sekta mbalimbali.

"Asilimia 25 ya bajeti ya Mfuko wa Maendeleo (USAID) unasaidia maendeleo ya Tanzania na kwa sasa tunakwenda kukaa kuangalia miradi ambayo tunasaidia Tanzania kwa kiasi gani inaendana na vipaumbele vya nchi hiyo (kilimo mifugo na uvuvi)," alisema.

Makamu wa Rais wa Kilimo, Watu na Maendeleo ya Jamii wa AfDB, Dk. Beth Dunford, alisema wataendelea kuisaidia Tanzania kifedha ili kuwezesha vijana, wajasiriamali na wakulima kukuza vipato vyao.

# 'Zingatieni lishe bora kukabili kansa'

**Na Renatha Msungu**

ILI kuipunguzia serikali mzigo wa kutibu magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari na shinikizo la damu yanayosababishwa na mpangilio mbovu wa vyakula, jamii imeshauriwa kuzingatia lishe bora katika familia.

Rai hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Maghembe, alipochangia mada katika mkutano wa masuala ya lishe na afya uliofanyika pembeni mwa Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Dk. Grace alisema serikali inatumia gharama nyingi kutibu magonjwa yasiyoambukiza yanayosababishwa na mpangilio mbovu wa vyakula, hivyo kila mmoja anapaswa kuangalia suala zima la lishe.

"Serikali inatumia gharama kubwa kutibu magonjwa yasiyoambukiza, hivyo kila mmoja anapaswa kulianga-lia hilo na wasisubiri serikali peke yake," alisema.

Naibu Katibu Mkuu alihimiza ifike wakati nchi za Afrika ziwe na mpango wa kusaidia kaya maskini kama ilivyo Tanzania, ili kuepusha utapiamlo.

Alisema kuna maeneo wanalima vyakula kwa wingi, lakini cha kushangaza mikoa hiyo inakuwa na tatizo la utapiamlo. Ni kutokana na kutokujua namna ya kupangilia mlo.

Alisisitiza elimu ya ulaji vyakula vyenye kuleta virutubisho izingatiwe. Jamii ipende kutumia vyakula vya asili na si chipsi na baga ambazo watoto wengi huzipenda.

Dk. Grace alisema lazima tuzijenge familia kula mlo kamili, ikiwamo kupanda mboga za majani badala ya kupanda maua peke yake.

Alisema jamii haiwezi kuepukana na lishe mbaya kwa kuisubiria serikali ihamasishe kula mlo kamili.

Kuhusu changamoto ya ugumu wa upatikanaji mlo kamili, Dk. Grace alisema serikali imeweka juhudi na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambayo ina mpango mahususi wa kunusuru kaya maskini, hivyo Afrika kwa ujumla ifike mahala kuwa na bajeti kwa ajili hiyo.



## HABARI KANDA KASKAZINI

# Serikali kusaka wafadhili kusaidia upatikanaji vifaa tiba

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amesema serikali imedhamiria kuendelea na mkakati wa kutafuta washirika wa maendeleo ndani na nje ya nchi ambao watawezesha upatikanaji wa vifaa tiba katika hospitali za wilaya.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wadau wa maendeleo kutoka Taasisi za Kimataifa ya Rotary 1918, Winndsor ya Canada na Taasisi ya PANETA, ambao wamesaidia upatikanaji wa mashine ya ultra sound na vifaa tiba vingine vya Sh. milioni 80 kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Siha iliyoko Mkoa wa Kilimanjaro.

"Tumekuwa tukiomba na tunaendelea kuwaomba wadau na washirika wetu wa maendeleo, watusaidie vifaa tiba katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kwa sasa kipaumbele chetu ni kwenye eneo la afya ya mama na mtoto, na Rais wetu (Samia Suluhu Hassan), anataka kupunguza/kumaliza vifo vya mama na mtoto nchini," alisema Dk. Mollel.

Dk. Mollel ambaye pia ni Mbunge wa Siha, alisema lengo la kutafuta na kisha kukabidhi vifaa tiba hivyo katika hospitali hiyo ni kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa kwa mama na mtoto.

Hospitali ya Wilaya ya Siha, inahudumia wakazi wanaoishi katika vijiji 60 vilivyopo wilayani humo, tangu ilipoanzishwa mwaka 2007 ikiwa kama kituo cha afya, baada ya vyama viwili vya ushirika kutoa ekari 40 za ardhi ili kujenga hospitali hiyo.

Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Christopher Timbuka, alisema vifaa vilivyopokewa vitasaidia kurahisisha matibabu kwa wanawake zaidi ya 350 ndani ya wilaya na wengine zaidi ya 80 kutoka nje ya wilaya, ambao wanaohudumiwa kila mwezi katika Hospitali ya Wilaya ya Siha.

Aliahidi kuwa vifaa tiba hivyo vitatumika kwa lengo lililokusudiwa la kuwahudumia wananchi wanaofika kutibiwa katika Hospitali ya Wilaya na si vinginevyo. "Ilikuwa nia yetu na itaendelea kubaki kuwa nia ya serikali, kwamba vifaa hivi visaidie kupunguza gharama za kufuata huduma katika maeneo mengine nje ya wilaya.

"Na sisi tutahakikisha kuwa tunavitunza ili viweze kuwahudumia watu wengi zaidi na watu waone manufaa ya vifaa hivi. Tunaishukuru sana diplomasia ya Rais Samia kwa sababu ndiyo inayotufanya tunakubalika kwa watu katika maeneo mbalimbali duniani."

Awali, Mwakilishi wa Taasisi ya Kimataifa ya Rotary 1918-Winndsor ya Canada, Dk. Andrea Cassidy, alisema lengo la kutoa vifaa hivyo ni kuhakikisha huduma bora na salama kwa mama na mtoto inapatikana bila kujali eneo alilopo mwananchi.




Ofisa Elimu Mkoa wa Arusha, Abel Mwaitupwa (wa tatu kushoto), akiangalia nyenzo za ufundishaji wa hesabu kwa njia ya vitendo, wakati wa ufunguzi wa warsha ya Chama cha Hisabati Tanzania (MAT), katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) jana. **PICHA: TUMAINI MAFIE**

# Ujenzi wodi za watoto njiti Manyara 'pasua kichwa'

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKATI Wizara ya Afya ikitangaza mpango wa serikali wa kuhakikisha hospitali zote nchini zinakuwa na wodi maalumu za uangalizi wa watoto njiti hadi ngazi ya jamii, katika Mkoa wa Manyara utekelezaji huo bado ni 'pasua kichwa'.

Akizungumzia tatizo hilo jana, Dk. Mathias Kimaro ambaye ni mbobezi wa uchunguzi wa watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo, alisema kati ya Aprili hadi Juni mwaka huu, wamezaliwa watoto njiti 35. Kati ya watoto hao saba walifariki dunia na katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Babati (Mrara), ikielezwa huzaliwa watoto njiti wanne mpaka sita kwa mwezi mmoja. Aidha, Dk. Kimaro, alisema kila mwezi mkoa huo unaweza kupata watoto njiti 10, huku akisisitiza kuwa licha ya kuwapo kwa idadi kubwa ya wanaozaliwa na hali hiyo bado wanaendelea kuishi bila tatizo.

"Chanzo cha kujifungua watoto njiti, ni upungufu wa damu wakati wa ujauzito, maambukizi ya njia ya mkojo au maambukizi ya njia za uzazi, kifafa cha mimba na kupata uchungu wa mapema.

...watoto njiti, huwa wanashindwa kunyonya, kwa sababu ubongo unakuwa haujatengeneza taarifa za kunyonya."

Juzi, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwa ofisi ndogo za wizara hiyo jijini Dar es Salam, wakati wa maandalizi ya awamu ya pili ya kuendelea kugawa vifaa tiba katika hospitali zenye wodi ya uangalizi maalum kwa watoto njiti alinukuliwa. Waziri Ummy alisema: "Tunataka hospitali zote nchini ziwe na huduma za uangalizi maalum kwa watoto njiti na tunashuka hadi ngazi ya msingi kama vituo vya afya, kwa kuwa asilimia 70 ya wanawake wajawazito, wanajifungua katika zahanati na vituo vya afya".

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, Rais Samia Suluhu Hassan, ameridhia kutumika kwa Sh. bilioni 6.3 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na kuanzisha wodi maalumu kwa watoto njiti.

## Serikali yaombwa kuajiri walimu wa Hisabati shule za msingi

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

CHAMA cha Hisabati Tanzania (MAT), kimeiomba serikali kuajiri walimu wa hisabati wengi katika shule za msingi kwa kuwa ndiko msingi wa somo hilo huanzia, licha ya kutokuwapo kwa motisha.

Inaelezwa kuwa kwa sasa shule za msingi nchini zinatishiwa na uhaba wa walimu wa somo hilo.

Akizungumza jana jijini Arusha, Mwenyekiti wa chama hicho, Betinasia Manyama, alisema shule za msingi zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa walimu wa hisabati.

Hivyo, aliitaka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kulichukua tatizo hilo na kuligeuza kipaumbele cha taifa kuelekea mapinduzi ya elimu.

"Unakuta shule ina wanafunzi 1,200 na ina walimu wawili, na kwingine unakuta shule ina wanafunzi zaidi ya 2,000 lakini walimu wa hisabati ni wanne. Bila kupepesa macho, walimu wa hisabati hawatoshi, kama taifa inabidi jambo hili liangaliwe upya,"alisema Manyama.

Aidha, alisema ni vyema pia kukawepo na motisha kwa walimu wanaofanya vizuri katika kutoa ufaulu kwenye somo la hesabu ili kuendelea kuwapa moyo walimu wanaofundisha.

Kuhusu kujengewa uwezo, Manyama, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuwaruhusu walimu wa hisabati, kuhudhuria mafunzo yanayoandaliwa na MAT, kila mwaka ili kukuza uelewa na kuendana teknolojia za kisasa katika ufundishaji wa somo hilo.

Naibu Mkuu wa Chuo, Mipango Fedha na Utawala wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Dk. Cairo Mwaitete, akizungumza katika warsha hiyo ya MAT, alisema hakuna namna Watanzania wanaweza kukwepa somo la hisabati, kwa kuwa kila kitu hutumia hesabu, hivyo ni vyema somo hilo likachukuliwa kwa uzito.

"Ukiwaambia watu kwamba Tanzania kuna umaskini toa takwimu ni wangapi wanapitia hali hiyo, anakisia. Tunaishi kwa kukisia kama kesho tutakuwepo, kila kitu lazima hesabu itumike. Kwa hiyo, hatuwezi kukwepa hesabu na ukikimbia hesabu umaskini unakufuata,"alisema Mwaitete.

Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, ambaye aliwakilishwa na Ofisa Elimu Mkoa wa Arusha, Abel Mtupwa, alisema wizara hiyo itaendelea kufanya kila aina ya jitihada ili kuhakikisha matatizo hayo yanatatulika.

Alisema warsha za mara kwa mara zitaendelea kutolewa kwa walimu kwa lengo la kuendelea kuongeza tija katika ufanisi wa somo hilo.





# Moto wateketeza mabweni Shule ya Msingi Mingasi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KUKATIKA mara kwa mara kwa umeme wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kumesababisha mabweni mawili ya Shule ya Msingi Mingasi iliyopo Kata ya Nyihogo Manispaa ya Kahama kuungua na kuteketeza vifaa vya wanafunzi.

Tukio hilo lilitokea Agosti 5 majira ya saa 12 jioni wakati wanafunzi wakijiandaa na maandalizi ya kuingia ndani kwa ajili ya kulala, kwamba genereta waliyokuwa wakiitumia kuzidiwa na kuwakata moto.

Mmoja wa mashuhuda walilieleza Nipashe kuwa muda mfupi baada ya kuingia bwenini kuliibuka moto mkubwa baada ya genereta lililokuwa likitumika shuleni hapo kuzidiwa.

Kidahi Njige alisema aliona moshi ukifuka kwenye mabweni na kuchukulia hali ya kawaida akijua wanafunzi wanafanya usafi kwa kuchoma takataka, lakini moshi ulizidi na kuamua kusogea na kubaini kuwa mabweni yanateketea na kuaamuru vijana aliokuwa nao kufika na kusaidia kuzima moto huo.

Alisema walifika na kuanza kuokoa wanafunzi waliokuwa ndani na vitu mbalimbali ikiwemo vifaa vya shule, sale na samani za ndani, huku wakisubiria Jeshi la Zima Moto na Uokoaji lililokuwa njiani kuja kusaidia kuzima moto huo.

Shuhuda mwingine, KeLvin Samweli alisema vitu vingi viliungua baada ya Jeshi la Zima Moto na Uokoaji kuishiwa maji na kuondoka kufuata maji mengine.

Alisema moto ulikuwa mkubwa licha wananchi kujitolea kuuzima lakini ilishindika na kuliomba jeshi hilo kuwa tayari kukabiliana na majanga, siyo kufika kwenye matukio wakiwa na maji machache.

"Tulifika shuleni hapa na kuokoa vyombo vya wanafunzi wanavyotumia kulia chakula, magodoro, masanduku na nguo zao lakini vitanda pamoja na vitu vingine muhimu tulishindwa kuviokoa baada ya moto kuwa mkubwa," alisema Samweli.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyihogo, Saidi Mitiming alikili kutokea kwa ajili hiyo, huku akisema chanzo chake bado hakijafahamika kutokana na kutokuwa na umeme katika mtaa huo tangu asubuhi mpaka jioni.

Naye Mkuu wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji wilayani Kahama, Mkaguzi Eduard Selemani alisema moto huo ulikuwa mkubwa na umeteketeza vitu vingi licha ya kuishiwa maji lakini walifanikiwa kuuzima na hakuna majeruhi yoyote aliyapatikana.

# Akamatwa tuhuma kuvamia makanisa mawili

**Na Said Sindo,** GEITA

JESHI la Polisi wilayani Chato linamshikilia, John Marore kwa tuhuma za kuvamia makanisa mawili ambayo ni Mtakatifu Bernadetha wa Lurd Parokia ya Nyakato-Buzrayombo na Kanisa la Waadventisti Wasabato yaliyopo Kata ya Buzrayombo mkoani Geita.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kutekeleza uhalifu huo usiku wa Septemba Mosi, 2023 na kusababisha Kanisa la Mtakatifu Bernadetha wa Lurd kufungwa kwa siku 30.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, Deusdedith Katwale amethibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo, akisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi kubaini wote waliohusika ili sheria ichukue mkondo wake.

"Sisi kama serikali tunaendelea na uchunguzi wa tukio hilo kubaini wote waliohusika ambapo mpaka sasa Jeshi la polisi linamshikilia mtu mmoja ambaye ni John Marore, lakini bado Jeshi la Polisi linaendela kutafuta wote walioshiriki katika tukio hilo," alisema Katwale.

Aliongeza kuwa hadi sasa hawajapata thamani kamili ya vitu vilivyoharibiwa katika makanisa yote mawili, huku akitoa wito kwa serikali za vijiji kuimarisha ulinzi shirikishi katika wilaya zote za Chato.

"Niombe wenyeviti wa vijiji, watendaji wa vijiji na kata kuhakikisha kwamba ulinzi shirikishi unaimarishwa, lakini pia niombe taasisi binafsi kwamaana ya taasisi ambazo zina miundombinu ya namna hiyo kuhakikisha pia wanaweka ulinzi wa kutosha kwenye maeneo yao ili kuepusha mambo kama haya ya watu ambao hawana nia njema na wananchi," alisisitiza.

Katika taarifa iliyotolewa Septemba Mosi na Makamu wa Askofu Jimbo la Rulenge -Ngara, Padri Ovan Mwenge ilieleza watu wasiojulikana walivunja ukuta wa kanisa na kufanya kufuru kwenye Sakramenti ya Ekaristi Takatifu kwa kuila ama kuondoka nayo na nyingine kuitelekeza sakafuni ndani na nje ya kanisa.

Kwa sasa waumini katika kanisa hilo wanasali nje, wakihimizwa kusali, kufunga, kufanya toba na malipizi kwa Mungu ili aboreshe mioyo ya watu wenye nia ovu kwa mambo matakatifu.

Waamini wa kanisa hilo, Anastazia Msuka na Severine Emmanuel walieleza kusikitishwa na tukio hilo na kusema kuwa kwa sasa inawalazimu kila mmoja kwa nafasi yake kuomba ili tukio hilo lisijirudie tena kwa kuheshimu nyumba za ibada na kutofanya vitendo visivyompendeza Mungu.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa maelekezo na Sheria ya Kanisa, Kanuni ya 1211 -1213 na kwa maelezo ya Askofu Severine Niwemugizi kanisa hilo litafungwa kwa siku 30, baada ya maboresho na ukarabati mdogo, litabarikiwa na kutakaswa ili liendelee kutumika.

Tukio hili ni la pili kutokea mkoani Geita ikiwa ni miezi sita imepita baada ya kijana mmoja Mkazi wa Geita kudaiwa kuvamia Kanisa Kuu la Kiaskofu Jimbo la Geita na kufanya uharibifu uliosababisha hasara ya Sh.milioni 48.2.



Takataka zikiwa zimerundikana bila ya kuondolewa katika Soko la Kambarage, Manispaa ya Shinyanga jana, kitendo kinacho hatarisha afya za wafanyabiashara na wateja sokoni hapo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanafunzi wapigwa 'stop' kushiriki ngoma za usiku

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa kike wanaotoka vijijini wameonywa kuhudhuria ngoma za usiku ambazo zimekuwa ni moja ya kichocheo cha kufanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kubakwa na kupata mimba.

Wito huo umetolewa juzi na Mshauri Mwelekezi wa mradi wa kupinga mimba na ndoa za utotoni kutoka Tume ya Taifa UNESCO, Dk. Rehema John, wakati akitoa elimu ya madhara ya ndoa za utotoni kwa wanafunzi wa kike kutoka Shule ya Msingi Ilola, Lyabusalu na Lyabukande wilayani Shinyanga.

Alisema kuna viashiria vingi ambavyo vimekuwa ni chanzo cha wanafunzi kufanyiwa vitendo vya ukatili, zikiwamo na ngoma za kimila hasa zile za usiku ambazo husababisha wanafunzi kubakwa na hata wengine kupewa mimba.


"Epukeni kutembea usiku, wala kuhudhuria sherehe za usiku na kwenye ngoma, sababu shughuli nyingi za usiku zinahatarisha usalama wa mtoto na kumuweka katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili," alisema Dk. Rehema.

Aidha, alisema vitendo vya ukatili dhidi ya watoto wa kike vinazuilika endapo watoto wenyewe na jamii wakawa na uelewa juu ya madhara ya ndoa za utotoni.

Hivyo, aliwataka wanafunzi wanapoona dalili za kufanyiwa vitendo vya ukatili wasikae kimya bali watoe taarifa mapema ili watua za haraka zichukuliwe na kuzuia ukatili usitendeke.

Naye Ofisa Elimu Maalum Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Irene Kisweka, aliwataka wanafunzi ambao wamepewa mafunzo hayo ya kupinga ukatili wakawe mabalozi wazuri kwa wenzao pamoja na kufikichua vitendo vya ukatili na siyo kukaa kimya.

Baadhi ya wanafunzi walisema elimu hiyo itakuwa msaada mkubwa kwao kufanya vizuri kitaaluma pamoja na kutimiza ndoto zao, huku wakisisitiza elimu ya kupinga ukatili na ndoa za utotoni wapatiwe pia na wazazi wao ili na wao waelimike.




Ukurasa 13

Hili la kuchimba dawa linahitaji dawa

Ukurasa 14



## Nje, ndani kinachokwamisha Darajala Mto Mirongo kubaki tatizo sugu

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 8, 2023
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe

# Inakosimama tafsiri ya Rais Dk. Samia, nafasi ya polisi nchini kubeba uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA wiki hii msamiati 'Dar inachemka kama bahari' imechukua nafasi yake. Kwanza kimataifa, kumekuwapo mkutano wa siku tatu ulioisha jana kujadili mustakabali wa chakula na biashara yake barani Afrika na hatima ya mlo barani Afrika sasa na siku zijazo.

Lingine, ni makamanda wa Jeshi la Polisi nchini nao wakakutana kwenye ukumbi wao, Oysterbay, Dar es Salaam safari hii wakijadili tija na majukumu yao.


Kwa namna ya pekee, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akawa mwenyeji kote, akianza na maafande, kisha akapaa na ndege hadi Nairobi Kenya, kujadili mazingira ngazi ya Afrika na dunia, ambako akapewa kipaza sauti kuwasilisha mada mwanana.

Siku ya pili tu, akawa amesharejea nyumbani kuwahi mjadala wa sekta yake kipenzi ya kilimo inayompa robo ya pato la taifa; theluthi mbili ya ajira ya watu; chakula kwa asilimia zote hadi ana ziada anataka kusitiri waliokosa nje kwa bei nafuu; bila kusahau utajiri wa malighafi kuwezesha viwanda nchini na nje.

Hapo kwenye chakula akawa mwenyeji wa hadhira zaidi ya watu 3,000, ila jana pia akawa na faragha na marais wenzake saba, wakikaa meza moja kujadili kilimo na chakula Afrika.

Hapo nako wakawepo majirani zake wa Afrika Mashariki ambao wapo mapema tu wakatua Dar es Salaam, kama vile jirani yake wa Burundi, Evarsite Ndayishimiye. Ama kweli 'kazi iendelee', Mama yuko kazini!

Akiwa Kurasini anaongea na



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea taarifa ya jeshi la Polisi, kutoka kwa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Camillus Wambura, mara baada ya kuwasili kwenye Bwalo la Maofisa wa Polisi, Oysterbay, Dar es Salaam, wiki hii. **PICHA; MTANDAO.**

maofisa wa Polisi, akawaasa kwa mambo kadhaa. Kwanza, akawakumbusha uaskari wao kubaki wakamavu mbali na vitambi, ujumbe ambao si mgeni.

Watangulizi wa awamu tofauti nao walishawahi kuyadokeza, lakini mara zote unagusa wengi, vyombo vya habari navyo kama kioo cha jamii wakaiweka mbele kwenye taarifa zao kwa umma, ukiwa ujumbe mzito.

Pili, Mama akalikumbusha Jeshi la Polisi nafasi yake inavyoweza kuchangia mipango ya maendeleo taifa, ambayo kimsingi wakitekeleza vyema, wanakuwa tayari wameshachangia kwa nafasi yao, Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

POLISI VS UCHUMI

Huenda mtu anaweza kupata utata wa kinadharia na uhalisia katika uhusiano wa polisi na maendeleo ya moja kwa moja kiuchumi.

Ufafanuzi wa kina wa Rais Dk. Samia, mtaalamu wa utawala wa umma na uchumi jamii, katika mazungumzo yake na makamanda wa polisi unabeba ishara ya uhusiano huo unaotegemea mchango wao askari.

Polisi ni nyenzo ya usalama wa raia na mali zake, inayotumiwa na utawala rasmi wa nchi kupata utawala bora. Pia, utawala bora ni msingi wa kupatikana demokrasia katika umma, hata kuwezesha kuwapo serikali iliyofanikiwa kiutawala

TAFSIRI ILIKOGOTA

Katika nadharia ya sayansi ya siasa, inaonyesha utawala ambao ni wa kiserikali unaendeshwa na kusimamiwa na nyenzo ya kisiasa. Hapo ndipo panapoonekana vyama vya kisiasa kuunda serikali, kuongozwa na sera ambayo ni tafsiri na nyenzo ya 'tunaendaje kiuchumi na maendeleo'.

Wanazuoni wa sayansi ya siasa kama vile David Easton na Harold Laswell, walitafiti na kupatia maana au tafsiri ya siasa, ikigota katika maana ya watu au mtu anavyosimamia umma na rasilimali zake, ambao kimsingi ndio uchumi.

Wachumi nao wakatafsri maana ya fani yao, kwamba ni kutumia rasilimali chache zilizoko kukidhi mahitaji mengi na nyeti, jamii hiyo ilivyo nayo.

Katika kile ambacho Rais Dk. Samia alikuwa akinena kwa hadhira ya maafande wa polisi katika mkutano wao, alibeba ujumbe wa utawala wa kisiasa kukidhi mahitaji ya kiuchumi kwa Watanzania.

Mara zote, ili kuwezesha hayo maono, siasa inarejea kwenye msaada wa nguvu za kiuchumi kuiwezesha kwa kutumia miundombinu ya serikali ambayo polisi ni sehemu yake, inatumika kufanikisha malengo yake.

Hapo sera za kisiasa zinahitimisha dira za kiuchumi na kijamii zinazopaswa kutekelezwa na mamlaka husika serikalini, zinazosimamiwa na sheria, pia mamlaka za kisheria.

Chochote ambacho serikali inalenga kufanikisha, jukumu la watekelezaji wakuu linarejea kwa umma ambao ndio wazalishaji, pia walipa kodi wakuu, ikizingatiwa nguvu kuu ya kiuchumi ya serikali kujiendesha iko kwenye kodi inayozalisha hata bajeti ya polisi.

Hiyo ndio inayoangukia, mathalani kauli ya Rais Dk. Samia akihimiza jamii ya Kitanzania kuchukua hatua kutekeleza malengo ya kisera, serikali ikiwapa mazingira bora ya kunufaika, ambako katika usalama wa mali na watu, polisi anapatikana.

INAENDELEA UK.12

SIMULIZI JEMBE LINALIPA...

# Aliyeitelekeza biashara mkaa, akihamia kwenye shamba, atamba hajutii maisha mapya ya sasa

## • Ajiongezea jukumu mwanamazingira kijijini 'mkaa hapana'

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

NCHINI sasa kuna jumla ya ekari 400,000 za misitu ya miti ya asili zinatajwa kupotea kila mwaka, kutokana na kukatwa kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa.

Ukame uliokithiri kutokana na ukosefu wa mvua, mito kukauka ni moja ya sababu zinazotokana na ukataji wa miti na hivyo kuwa chanzo cha mabadiliko ya tabianchi.

Ukosefu wa mvua inatajwa kuwa moja ya visababishi vya njaa kutokana na wananchi kukosa mavuno, kwa sababu ya ukame na imekuwa ikisababisha baadhi ya nchi kuwa na wakimbizi wanaokimbia ukame kwao kwa kukosa chakula.

Mnamo Juni 30 mwaka huu, Muungano wa Mashirika katika eneo la Kalehe Jimboni Kivu Kusini Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wako katika harakati za kuhamasisha wananchi kupanda miti kupambana na mabadiliko ya tabianchi baada ya eneo hilo kukumbwa na mafuriko yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mazingira.

Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, imeendelea na kampeni katika maeneo mbalimbali nchini kupanda miti, wakishirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania.

Kampeni hiyo inaenda sambamba na kudhibiti ukataji miti na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kama nishati ya kupikia, badala yake kutumia zaidi gesi na umeme.

Biashara ya mkaa inatajwa itapungua, endapo watumiaji wengi watahamia matumizi ya nishati safi na hiyo itafanikiwa kupitia elimu ya faida ya matumizi ya nishati ya gesi, pia kuwa na mashuhuda watakaotumika kama mabalozi.

**ULIVYO USHUHUDA**

Ni simulizi inayomhusu, Juma Chambwewe mfanyabiashara aliyecha biashara hiyo na kuhamia kilimo, ambaye sasa ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Mnindi Kata ya Vigwaza katika Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo.



Juma Chambwewe,mfanyabiashara wa mkaa, aliyehamia kilimo , sasa akiwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mnindi, Kata ya Vigwaza katika Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani. **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

Kabla ya kuwa Mwenyekiti wa Kijiji hicho mwaka 2014, Chambwewe alikuwa mfanyabiashara mkubwa wa mkaa ambao, alikuwa akiuza katika jiji la Dar es Salama, kituo chake kikubwa kikiwa Magomeni.

Anataja kuwa biashara aliyoanza kuifanya zama za miaka ya 1990, alikuwa anatoka jijijini Dar es Salam na kwenda maeneo ya Lugoba Porini, Bagamoyo kusaka mkaa ambao alikuwa ananunua gunia kwa shilingi 100 na kuuza kwa shilingi 400.

Chambwewe anasema, ameendelea na biashara hiyo kwa muda mrefu akienda kwenye mapori tofauti kufuata mkaa na kuusafirisha hadi katika kituo chake alichotumia kuuza, Magomeni.

Anatamka, hivyo ilipofika miaka ya 2000 baada ya kukumbana na tatizo ambalo lilisababisha kumaliza mtaji aliokuwa nao, alalazimika kurudi kwenye eneo lingine Vigwaza na Kwala, Bagamoyo, kufungua mapori kwa kukata miti na kuichoma mwenyewe, anapeleka mkaa sokoni.

Chambwewe anasema haikuwa rahisi kwake kuanza upya, lakini akafanikiwa kumiliki mashine zaidi ya mbili, ambazo alizitumia kukata miti kwa urahisi na kuchoma mkaa kazi iliyomuwezesha kusafirisha gari moja na zaidi kila siku lililosheheni mkaa na kwenda kuuza Dar es Salaam.

"Nilianza kununua gunia la mkaa kwa Shilingi 50 pamoja na malipo mbalimbali hadi kulipakia gunia kwenda Dar es Salaam, nilikuwa nimetumia sh. 100 kwa gunia moja niliendelea hivyo, hadi nilipoanza kuchoma mwenyewe na kusafirisha yaani gunia lilipofikia kuuzwa kwa shilingi 12000 porini lakini sikuweza kuwa na mafanikio ya aina yoyote"

Anaeleza kuwa, pamoja na fedha nyingi alizokuwa akipata katika biashara hiyo, lakini hakuyaona mafanikio kwa kipindi cha zaidi ya miaka 10 akikata miti na kuuza mkaa.

**AHAMIA KWENYE JEMBE**

Baada ya kupata nafasi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mnindi, katika Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani, akaamua kuachana na kazi hiyo na kuanza kilimo ambacho kwa sasa anajivunia kwa kupata mafanikio.

"Kabla ya kuanza kuingia kwenye kilimo nilifanya utafiti kati ya watu 20 wanaojishughulisha na mkaa hakuna aliyeeleza kuwa na mafanikio, badala yake fedha hizo zinaishia kwenye kufanya mambo madogo pamoja na fedha nyingi wanayoipata" anasema.

Anafafanua kuwa, hapo ndipo akaamua kuhamia kwenye kilimo baada ya utafiti wa manufaa yake.

"Ukitaka kufanya kazi hakuna maendeleo na kila siku wanauza mkaa na kuharibu mazingira, kazi ya kukata miti fedha yake haina baraka ninachowashauri ni kuangalia upande wa kilimo ambacho nimeshuhudia mafanikio yake kwa muda mfupi" anafafanua.

"Nimeanza kilimo na ufugaji bora na mpaka sasa nina ng'ombe zaidi ya 100, mbuzi zaidi ya 200, mahindi nimelima zaidi ya ekari 100, alizeti na maharage na kwa msimu huu pamoja na kuwa mgumu, lakini natarajia kuvuna zaidi ya gunia 500, maharage gunia 50 hadi 80 na alizeti hadi sasa nimeshavuna gunia 70" anaeleza.

Mwenyekiti huyo anasema, kaanzisha mashamba kwa ajili ya kupanda miti na katika maeneo ya kijiji chake, amekuwa akiendeleza upandaji miti kutunza mazingira.

Anasema, wapo wanaoeleza kikwazo kwenye kilimo kuwa ni mitaji, jambo ambalo yeye anapinga kwa hoja mtu akiamua kuingia shambani, hata mtaji mdogo alio nao unaweza kuwa mkombozi kwake, badala ya kuendelea kuuza mikaa.

Sasa anajitambulisha kuhamasisha matumizi ya gesi na kuachana na kuni katika eneo lake, akiendelea na harakati za kutunza mazingira katika kata ya Vigwaza anakoishi, kwenye kitongoji cha Mbala Kijiweni, ambako wao wameamua kuunda Kamati ya Kudhibiti Ukataji Miti ovyo.

Saitot Lecope, ni mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, anaeleza kuwa wameanza kufanya kazi yao Septemba,2022 na wamekuwa wakizungukia katika mapori ya karibu na kitongoji hicho na kuwakamata wanaovuna miti bila kibali.

Anasema, kwa sasa katika kitongoji chao wanasaka wanaopitisha mkaa kupeleka Dar es Saalam na kwamba wanaendelea na utaratibu huo hadi pale watakapoona biashara hiyo imekoma katika kijiji chao.

Kwa mujibu wa Lecope, elimu ya matumizi ya nishati ya gesi inahitajika zaidi kwa wananchi na kwa kufanya hivyo itasaidia kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa katika maeneo ya Vijijini.

**TAKWIMU KITAIFA**

Novemba Mosi mwaka jana, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akabainisha takwimu nchini zinaonyesha kuwa kaya zinazotumia nishati ya gesi ni asilimia tano, huku asilimia tatu wanatumia umeme.

Katika mkutano huo Rais Samia, anasema katika bajeti ya 2023/2024 Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia .

Akizindua kampeni ya Matumizi ya Utunzaji Mazingira na matumizi ya Nishati Mbadala kwa mkoa wa Pwani iliyofanyika Aprili 19 mwaka huu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dk. Selemani Jafo, akazielekeza taasisi na shule za bweni kutumia gesi badala ya mkaa na kuni.

# Inakosimama tafsiri ya Rais Dk. Samia, nafasi ya polisi nchini kubeba uchumi

**INATOKA UK.11**

Mkulima wa mwekezaji wa kigeni anapokuwa katika amani na utulivu unaosimamiwa na polisi iliyojitosheleza kwa vifaa, stadi na mafunzo, nidhamu na utii, ikiwapa ushirikiano ikiwamo kupitia 'Polisi Jamii', maana yake umma huo unapewa nafasi kuzama zaidi kuzalisha mali na shughuli za maendeleo.

Zao lake, mara moja kunakuwapo tija za uzalishaji, kodi inakuwa juu, ajira na kukua miundiombinu ya kimaendeleo.

Kwa maana hiyo, ili uzalishaji ufanyike, kunahitajika kigezo muhimu cha kuwapa amani na utulivu jamii kiujumla, kufanikisha malengo ya kisera na nje ya sera.

Hapo, mamlaka hiyo ya Polisi na wadau wengine wa usalama wanapaswa wawe na sifa ya uwezo kifania na 'kukubalika' inayohimizwa katika sayansi ya siasa na ndio maana kuna ubia wa umma kama 'Polisi Jamii,' umma unakuwa sehemu ya chombo hicho.

Hapo inarudisha ukweli wa jambo katika hatua kadhaa za nadharia zilizotafitiwa kwamba sifa ya serikali kukamilika inapaswa 'kukubalika mbele ya umma wake' hata kuisogeza jirani na demokrasia ambayo inatafsiriwa ni " utawala wa watu, kwa ajili ya watu na kwa ajili ya watu."

Vilevile, katika umma huo, pia jamii ina wajibu wake ambao Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, katika kuunda Taifa changa la Tanzania mwaka 1964, alitamka kwa kizungu 'It Can Be Bone, Part Your Part' akimaanisha 'inawezekana timiza wajibu wako.'

Ujumbe huo unaigusa zaidi umma nayo katika nafasi yake, kulinda amani na utulivu, kuheshimu sheria na kutoa ushirikiano kwa vyombo vya usalama kama polisi ikiwamo katika harakati kama za 'Polisi Jamii'; maana pande mbili, serikali na umma, kila moja ina haki na wajibu wake kwa ng'ambo ya pili; ni wangapi wanatii sheria, bila ya shuruti?

Ni mara moja penye nyendo za ushirikiano huo, harakati za uchumi wa kijamii zinakuwa zinapiga hatua nchini, wawekezaji kimataifa nao wanavutiwa kufika nchini kuingiza mitaji yao, sera na mipango ya maendeleo kitaifa inaenda kama ilivyopangwa na ndicho Dk. Samia anakipigania.

Polisi, kama walivyo askari wengine, moja ya sifa yao kuu ni utii na nidhamu, ukakamavu na stadi za mapambano katika kutimiza majukumu yao ya msingi na ziada.

Hapo ndipo inapokuja nafasi ya ukumbusho wa Rais Dk. Samia, akiwatamkia msamiati 'vitambi'; wawe tayari na imara kitaaluma kusimamia amani na utulivu, ikiwamo usimamzi wa usalama kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mwaka ujao, pia Uchaguzi Mkuu mwaka unaofuata 2025.

Polisi kufanikisha amani katika chaguzi tajwa zinazokuja, kuna maana imechangia kuwapo utawala bora, pia kukubalika kiserikali katika kigezo hicho cha kidemokrasia.

Nadharia na uhalisia unaainisha, pale kunapokuwapo amani, utulivu na kukubalika kiserikali, unahamasisha uchumi nchini kiustawi, kupitia nadharia ya kiuchumi iitwayo 'multiplier effect', kwa maana ya ufanisi wa ngazi moja, unazaa mafanikio mengine kiuchumi. Hapo amani na demokrasia, inakuwa imezaa ustawi wa kiuchumi, nyayo za polisi zikishuhudiwa.


Katika msimamo wa kisera ulioko sasa nchini kuvutia mitaji nchini, maana yake jeshi hilo ambalo Rais Dk. Samia amelipatia neno wiki hii, linakuwa limechangia kumiminika mitaji ya kigeni nchini kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi nchini, ikiwamo sekta ya viwanda inayopigiwa debe. Hadi sasa kuna ushuhuda.

Kwa mfano, kuwapo mkutano mkubwa wa kilimo barani Afrika ulioisha jana nchini, hadi Tanzania kukubalika kuwa mwenyeji wake, suala la uhakika wa amani ambalo liko kwenye dhamana kuu ya polisi na vikosi vingine vya ulinzi na amani, inakuwa imechukua nafasi yake.

Hiyo nayo ni 'multiplier effect' ambayo polisi inajivunia mkono wake chini ya Rais Rais Dk, Samia, Amiri Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama nchini.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hili la kuchimba dawa linahitaji dawa




**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

BINADAMU na wanyama kimaumbile wanafanana kwa kiwango kikubwa sana, kwani wote wana mahitaji ya msingi ya kula, kunywa, kupumzika na hata kujisaidia haja ndogo na kubwa.

Wakati binadamu hutafuta na kutenga maeneo muhimu ya kukidhi haja zake, wanyama hufanya hivyo kokote waliko, bila kujali muda wala eneo.

Kutokana na utofauti huo, binadamu amejenga hulka ya kuchukia kinyesi chake na hata haja ndogo yake, tofauti na mnyama, ambaye anaweza kulalia kinyesi hata mkojo wake.

Inapotokea binadamu amejisaidia mathalani chumbani au kitandani, huonekana wa ajabu na kuitwa majina na ndiyo sababu sehemu zingine kindumbwendumbwe hulizwa.

Mtu anapoitwa kikojozi, huonekana kudhalilika sana, kwamba anaishi na uchafu au anaweza kulala nao, ndiyo sababu watoto wengi huchapwa na kuadhibiwa kwa kujisaidia vitandani.

Kwa mnyama, hilo halipo na ndiyo sababu binadamu anapopata kinyesi cha mnyama hushukuru na kukigeuza kama mbolea au udongo wa kukandikia nyumba yake.

Kwa kuwa wanyama huishi maporini na kujisaidia huko, hatujawahi kusikia binadamu wakilalamika, kwamba wanyama wanachafua mazingira.

Lakini, binadamu anapoonekana kujisaidia porini, huonekana anachafua mazingira, ila tukijiuliza tofauti ya uchafuzi anaofanya binadamu na ule ambao hauonekani kufanywa na mnyama, ni kitendawili.

Bila shaka kinyesi si chakula, kiwe cha mnyama au binadamu, hivyo kinyesi ni kinyesi tu bila kujali kinatolewa na kuhifadhiwa wapi, na vyote vinaweza kutumika kama mbolea na kuwekwa shambani.

Baadhi ya mataifa ya Mashariki ya mbali, yamekuwa yakitumia si tu kinyesi cha wanyama, bali hata cha binadamu kama mbolea kwenye mashamba yao, na kuonekana kuwa na tija sawasawa.

Hivi sasa Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) limelazimika kuja na adhabu ya shilingi milioni tano kwa dereva wa gari atakayebainika amesimamisha gari lake porini na kuruhusu abiria kujisaidia-kuchimba dawa.

Bila shaka NEMC inatimiza majukumu yake ya msingi kwa kutaka kuhakikisha, kwamba mazingira yanahifadhiwa kwa njia yoyote ile kulingana na sheria inavyowaongoza.

Imekuwa ikifanya hivyo hata pale ilipoamua kupambana na makelele na mitetemo kwa kufungia baadhi ya majumba ya starehe, huku uamuzi huo ukipingwa na baadhi ya wanasiasa.

Hili la sasa dhidi ya uchimbaji dawa maporini, linakuja, lakini nalo litakumbana na upinzani ambao naweza kusema ni wa asili, kwani haja kubwa na ndogo hazipangwi, bali hutokea kimaumbile.

Mtu anapojikuta katika hali hiyo akiwa safarini, anatarajiwa afanye nini hasa akiwa katika gari lisilo na choo. Akiingia porini huko kujisaidia anavunja sheria ndiyo, lakini afanye nini wakati amebanwa kimaumbile.

Kuna baadhi ya wazee au wagonjwa ambao si rahisi kuvumilia kubana haja mpaka eti afike sehemu zenye maeneo ya kujisaidia mathalani hotelini, akijisadia kwenye mavazi akiwa ndani ya basi, itakuwaje?

Yapo mabasi ndiyo, yenye vyoo ndani, lakini abiria hutangaziwa kuwa vyoo vilivyopo si kwa ajili ya haja kubwa bali ni ndogo tu, je, wenye haja kubwa na waliobanwa wafanyeje, hasa ikizingatiwa hiyo milioni tano hawana?

Kama mnyama akijisaidia porini hachagui mazingira, iweje binadamu akifanya hivyo anachafua mazingira? Tunataka kujiaminisha hivyo, wakati Dar es Salaam tunashuhudia bomba kubwa linalomwaga majitaka baharini.

Hivi bomba hilo kumwaga majitaka baharini si uchafuzi wa mazingira kweli? Je, samaki wanaoliwa na binadamu ilhali wamevuliwa kwenye bahari inayomeza majitaka ya Jiji lote kama Dar es Salaam, si wachafu kimazingira?

Ili kuendana na hali ilivyo hasa katika kuisaidia NEMC kupambana na wachafuzi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kuondokana na uchimbaji dawa porini, halmashauri za miji na wilaya husika yanamopita magari ya abiria zijipange.

Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha zinajenga maeneo ya abiria kujisaidia, ili kuondokana na tabia hiyo ya kujisaidia porini, ingawa ni kweli kuwa hakuna anayejisaidia katika vyanzo vya maji.

Lakini, pia ni ukweli kuwa haja ndogo na kubwa za binadamu na wanyama ni mbolea kwa mimea, iliyopo kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, ndiyo sababu maporini pamoja na wanyama kula majani, bado yanastawi kutokana na mbolea ya kinyesi chao.

Lakini, kwa NEMC nashauri iondokane na dau la Sh 500,000 kwa mtu atakayepiga picha watu wanaochimba dawa, kwa sababu kufanya hivyo ni kosa kisheria, kumpiga mtu picha akijisaidia kwani ni kuingilia faragha.

Tukabiliane na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kuja na suluhu badala ya kuja na adhabu zisizowezekana kwa Watanzania wasio na uwezo wa kusafiri kwa ndege, kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Alamsiki!

UCHUMI

# Nje, ndani kinachokwamisha Daraja lililoko Mwanza kubaki tatizo sugu

**Na Anthony Gervas, MWANZA**



Mwonekano wa daraja la mto Mirongo lililopo Mabatini jijini Mwanza, ambalo chini limeziba taka zinazosababisha kuzuia maji kupita kirahisi nyakati za mvua. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

NI siku kadhaa zilizopita ilikuwa Jumanne, saa tano asubuhi,nilipobisha hodi katika ofisi ya Wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Mwanza (TANROADS), kwa ajili ya 'jambo langu' kihabari, kuhusu changamoto ya Daraja Mto Mirongo lililopo Mabatini, jijini hapa.

Baada ya kufika ofisini, nilikutana na Meneja wa Tanroads Mhandisi Ambrose Pascal, ofisini kwake akihitaji kulitambulisha 'jambo langu', nami nikamwambia kuzungumza naye kuhusu changamoto za daraja hilo, ambalo muda mrefu limekuwa likilalamikiwa kusababisha athari.

Mhandisi Pascal akanielekeza kuwa nimuone Mhandisi Mkuu wa Tanroads Mkoa, Mhandisi Ramadhan Majaliwa, akitamka. "Muone Mhandisi Rama (Ramadhani Majaliwa), mimi nimeitwa kwenye kikao na Mkuu wa Mkoa ndiko nakwenda."

Hivyo nikabadili mwelekeo kwenda kumuona Mhandisi Majaliwa aliyeridhia kufanya mazungumzo naye kuhusu suala hilo, akifafanua zaidi kilichopo nyuma ya pazia

Hilo ni daraja limeunganisha barabara kuu ya Musoma hadi nchi jirani ya Kenya, pamoja na Uganda, hivyo limekuwa likikumbwa na mafuriko ya maji nyakati za masika na kusababisha pia magari na vyombo, hata kwa watembea kwa miguu kushindwa kupita, hali inayosababisha msongamano mkubwa wa vyombo hivyo.

Uzoefu ni mvua zinaponyesha, mahali hapo hujaa maji kupita kiasi, yakisambaa hadi makazi ya watu, kupita juu ya daraja, uharibifu wa mali na mifugo. Sio ajabu kusikia mikasa hatari, maisha na vitu vingine vya thamani kusombwa na mafuriko hayo, kuelekea Ziwa Victoria.

Marejeo hayo na dodoso za kihabari, zikamfikisha mwandishi wa makala hii na bosi wa TANROADS Majaliwa, kuingia katika faragha ya dakika 15 ya mazungumzo. Yakawa kama ifuatavyo:

**SWALI**: Mhandisi Rama(Ramadhani Majaliwa) unalifahamu Daraja la Mto Mirongo Mabatini na changamoto zake.?

**JIBU:** Ndiyo nalifahamu liko chini ya usimamizi wetu TANROADS Mkoa wa Mwanza.

**SWALI:** Je unazifahamu changamoto zake kwa wananchi, ambazo hulalamikiwa kila mara kukumbwa na mafuriko ya maji nyakati za mvua, pia kusababisha magari, bajaji, pikipiki na watembea kwa miguu kushindwa kupita ?

**JIBU:** Ndiyo, mara nyingi mafuriko hayo ya Maji Mto Mirongo husababishwa na wananchi wenyewe ambao wanatakiwa kuacha kutupa taka kwenye mto huo, zinazosababisha kuziba katika matoleo ya maji kwenye daraja hilo, hivyo wao ni sehemu ya kisababishi hicho.

Wananchi wamekuwa kisababishi na chanzo kikubwa uchafuzi mazingira katika mto huo, kutokana na utupaji taka ambazo nyakati za mvua husafirishwa hadi kwenye daraja hilo na kuziba mapitio ya maji, hivyo kusambaa kwenye makazi yao, huku mengine hupita juu ya Daraja yakifunga barabara, anasema Majaliwa.

Pia, daraja hilo chini yake kuna miundombinu ya mabomba ya maji, ambayo huchangia kuzuia taka kupita katika matoleo ya maji, kwa sababu makubwa yanatakiwa kuhamishiwa sehemu nyingine, ili kupisha upanuzi ule.

**SWALI:** Upanuzi wake unatarajia kuanza lini ili kuondoa adha hiyo kwa wananchi wa jiji hili na mkoa kwa ujumla?

**JIBU:** Kwanza Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA), wanatakiwa kushauriwa ili waweze kuhamisha mabomba hayo ambayo ni makubwa yanayosambaza maji kwa wananchi,ambayo yamepita chini ya daraja hilo.

Upanuzi wa daraja hilo utakwenda sambamba na upanuzi wa barabara kuu ya lami kilomita 36 kutoka Nata mjini hapa hadi Nyanguge wilayani Magu, itakayopanuliwa kwa njia nne.

Hivyo, miundombinu hiyo ikikamilika itachochea uchumi, utalii na maendeleo ya wananchi, kwa hiyo tunasubiri serikali itakapotenga bajeti ya ujenzi wake, ila tayari usanifu wa upanuzi huo ulishafanyika.

SWALI: Mtandao wenu wa barabara za lami ni kilomita ngapi?

JIBU: Mtandao wetu wa barabara hizo uko kilomita 258.74. Pia, tunatarajia kujenga upya barabara kuu ya lami kutoka jijini hapa, hadi mkoani Shinyanga yenye urefu wa kilomita 104, tunasubitri kutengewa bajeti ya Serikali.

**MWAUWASA.**

Meneja Uzalishaji na Usambazaji Maji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (MWAUWASA) jijini Mwanza, Mhandisi Robert Lupoja anasema kama kuna mradi unaoendelea wa ujenzi wa daraja hilo na barabara kuu ya lami, wako tayari kuhamisha mabomba hayo baada ya kuwasiliana na TANROADS kwa barua, kwa sababu ndiyo wahusika wakuu wa mradi huo.

"Sisi tutaweza kuhamisha mabomba yetu kama kuna upanuzi wa Mradi wa Daraja na Barabara unaendelea, tuna mabomba makubwa matano yenye ukubwa wa milimita 500, 200 na 300 ambayo husambaza maji, kwa sababu Tanroads ndiyo wanaogharimia mradi huo,' anasema Mhandisi Lupoja.

Pia, anafafanua hakuna kitakachoharibika kuhamisha, ukifika wakati wa kuanza mradi ili kuachia hatua zingine za maendeleo ziendelee kufanyika, lengo ni kupata huduma stahiki kwa wananchi.

**TARURA YACHEKELEA**

Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wilaya ya Nyamagana, unasema serikali kupitia Ufadhili wa Benki ya Dunia(WB) wamepata Mradi wa Uboreshaji Mto Mirongo,ili kuzuia Mafuriko kwa wananchi katika Daraja hilo pamoja na kupendezesha jiji la Mwanza.

Meneja wa Tarura Wilaya hiyo,Mhandisi Dastan Kishaka anafafanua kuwa Benki ya Dunia(WB) imetoa ufadhili wa fedha kwa ajili ya Mradi wa Uboreshaji Mto Mirongo, ambao hupeleka maji yake Ziwa Victoria, ikiwa mradi huo kwa ujumla unakusudia kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 15.

Kishaka anaeleza, kwamba katika Mto Mirongo takribani kilomita 6.8, utajengwa kingo zake na kuwekwa vituo vidogo vidogo vya mapambo ili iwe sehemu ya vivutio vya utalii wa wananchi jijini hapa na maeneo jirani, ikiwa usanifu wake umeshakamilika kufanyika mwaka huu, wakisubiri serikali kuwapa fedha za kuanza kazi hiyo chini ya usimamizi wao na jiji.

Vilevile anasema, TARURA inatambua uwepo wa changamoto ya daraja la mtaa wa Uhuru, ambalo ni tatizo kubwa wakati wa masika vyombo vya usafiri yakiwemo magari, bajaj, pikipiki na wapitao kwa miguu hushindwa kuvuka, kutokana na kufurika maji ambayo hupita juu ya daraja hilo na kusababisha adha kubwa kwa wananchi.

Hata hivyo Mhandisi Kishaka anaeleza, kuwa kimsingi jiji la Mwanza, hutakiwa kutoa asilimia 10 ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuiwezesha TARURA katika ujenzi wa Barabara zake ziweze kupitika kutegemea bajeti husika, ikiwa mwaka jana walipata bajeti ya shilingi bilioni 1.8, lakini Serikali ilitoa shilingi milioni 660, mwaka huu bajeti yao imeongezeka hadi kufikia bilioni 2.2.

Anadai kuwapo changamoto za wananchi kuharibu miundombinu ya barabara, wakiziba mitaro, alama za barabarani, kuiba vibao akiwataka kuacha tabia hiyo, huku akimshukuru Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, kuwaongezea bajeti za tozo na Mfuko wa Jimbo awali walipata shilingi bilioni tatu na sasa imefikia takribani shilingi bilioni 7.





Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) wilaya ya Bahi, Justine Sangulah (wa pili kulia), akizungumza wakati wa kikao cha baraza la umoja huo wilaya, eneo la Bahi sokoni, mkoani Dodoma juzi. Wa (tatu kulia) ni Mbunge wa Bahi, Keneth Nollo.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Viongozi uhifadhi wanyamapori wapewa mafunzo maalum

**Na Valentine Oforo,** SINGIDA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeendelea kuimarisha shughuli za uhifadhi nchini kwa kutoa mafunzo maalumu kwa viongozi wa Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori (WMAs) katika Wilaya ya Waga mkoani Iringa na Chamwino mkoani Dodoma.

Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea viongozi hao uelewa wa pamoja juu ya umuhimu wa kusimamia rasilimali za wanyamapori, hasa katika maeneo ambayo wananchi wametenga maeneo yao kwa ajili ya kupisha shughuli za uhifadhi.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo hayo yanayofanyika mkoani hapa, mwakilishi wa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Rose Mdendemi alisema mafunzo hayo yamejikita kuwapa viongozi hao uwezo wa kuendeleza shughuli za uhifadhi kwa uweledi, ikiwa ni pamoja na kusimamia rasilimali katika maeneo ya jumuiya hizo.

Mafunzo hayo yamewezeshwa na Mradi wa Kudhibiti Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (IWT - PROJECT).

Mradi huo endelevu unatekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na unalenga kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi nchini, kudhibiti ujangili, kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu, pamoja na kuhakikisha wananchi wananufaika kupitia shughuli za utalii.

Aidha, alishukuru Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), kwa mchango mkubwa wanaoutoa kwa Wizara katika kutekeleza majukumu hayo.

"Tunaamini mafunzo haya yatawezesha wananchi kusimamia rasilimali hizi vizuri na hatimaye kufikia malengo ya kuinua uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla."alisema

Naye, Rachel John, Ofisa Wanyamapori Mkuu kutoka Wilaya ya Mufindi na Ofisa Wanyamapori Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma, Yusuph Nyonyi, waliishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuwezesha kufanyika kwa mafunzo hayo ambayo ni muhimu katika jamii zilizotoa maeneo yao kwa ajili ya shughuli za uhifadhi.

Mwakilishi kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Damas Masologo alisema ni matarajio yao kuwa mradi utapokuwa umekamilika jumuiya mbalimbali za wanyamapori nchini zitakuwa zimesimama vizuri hasa katika kutekeleza majukumu yao.

# Mkakati kunusuru vyanzo vya maji Makutupora waanza

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na ongezeko kubwa la matukio ya moto katika hifadhi ya vyanzo vya maji Makutupora jijini Dodoma unaosababishwa na shughuli za kibinadamu, uongozi wa bonde la Wami/Ruvu umeanzisha mkakati wa kuweka vikinga moto ili kulinda miundombinu ya uzalishaji maji katika eneo hilo.

Mkurugenzi wa Bonde la Wami/Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmassy, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri kukagua uwekaji vikinga mto katika hifadhi hiyo ya vyanzo vya maji.

Alisema kutokana na matuko ya mara kwa mara ya moto katika hifadhi hiyo wameamua kuweka vikinga moto ili kulinda miundombinu na vyanzo vya maji katika eneo hilo linalotegemewa kwa zaidi ya asilimia 90 kuhudumia wakazi wa Dodoma.

Mmassy, alisema pamoja na kuweka vikinga moto lakini pia watashirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuendesha doria kwenye eneo hilo ili kuzuia matukio ya watu kuchoma moto katika eneo hilo.

"Hifadhi hii ya vyanzo vya maji ipo chini ya Bonde la Wami/Ruvu na chanzo hichi ni chanzo muhimu sana ambacho kinategemewa kwa asilimia 90 ya uzalishaji wa maji katika Jiji la Dodoma" alisema

Aidha, alisema lengo la kuweka vikinga moto katika eneo hilo ni kupunguza athari ambazo zimekuwa zikijitokeza katika hifadhi hiyo ya vyanzo vya maji.

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Donasiano Shamba, alisema matukio ya moto ambayo yamekuwa yakitokea katika hifadhi ya vyanzo vya maji yanasababisha uharibifu miundombinu ya uzalishaji maji.

# CMSR, Serikali waungana kuboresha afya ya mama, mtoto

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la CMSR-Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya limedhamiria kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto kwa kununua vifaa tiba muhimu.

Vifaa hivyo ambavyo vitatumika kuwahudumia watoto wachanga na kinamama katika kipindi cha ujauzito na wakati wa kujifungua.

Meneja msaidizi wa mradi wa kupunguza vifo vya watoto wachanga na kinamama unatekelezwa na shirika hilo, Dk. Hamoud Ndenge alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha uzinduzi wa mradi huo.

Mkutano huo uliwashirikisha wawakilishi kutoka Wizara ya Afya Tanzania Bara na Zanzibar, TAMISEMI, na wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya CUAMM, COPE, AVSI na AICS.

Dk. Ndenge, alisema shirika hilo pia litasaidia kutoa mafunzo kwa watoa huduma za mama na mtoto ili kuwajengea uwezo wataalam hao kupitia mradi huo unaojulikana kwa jina la IMaNHC.

Alisema, mbali na ununuzi wa vifaa, shirika litawajengea uwezo madaktari na wauguzi wanaotoa huduma za mama na mtoto kwenye wodi za watoto wachanga, kliniki ya wajawazito na wanapojifungua.

Alisema kuwa vifaa vitakavyonunuliwa vitawezesha kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma ya mama na mtoto inayotolewa katika vituo vilivyo kwenye mradi huo.

Alisema kuwa mradi huo pia unashirikisha nchi za Kenya na Uganda kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa masuala yanayohusu afya kwa ujumla na kubadilishana uzoefu miongoni mwa wataalam katika nchi hizo.

# Serikali yawatoa hofu wakulima upatikanaji mbolea

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema imepanga kuongeza usambazaji wa mbolea nchini, kwamba septemba mwaka huu wakulima wote watakuwa wameshapata ili waanze maandalizi ya kupanda.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, aliyasema hayo jana alipotembelea ofisi za kampuni ya mbolea ya Yara Tanzania, kusema serikali itashirikiana na kampuni hiyo kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa wakati.

"Wizara ya Kilimo imepanga kuongeza usambazaji wa mbolea, ndiyo maana usambazaji wa mbolea unaanza mwezi huu ili iwafikie wakulima haraka," alisema Silinde na kuongeza:

"Uzalishaji ni mchakato na kuna mikakati ya muda mfupi na mrefu, kwa hiyo mkakati wa muda mrefu ni pamoja na kujenga kiwanda na mkakati wa mfupi ni kusambaza mbolea".

Rais na Mtendaji Mkuu wa Yara International, Sven Tore Holsether aliishukuru serikali ya Tanzania kwa kuonyesha ushirikiano tangu walipoanza kazi nchini mwaka 2004.

Alisema lengo la Yara ni kuimarisha upatikanaji wa chakula, ndiyo maana wanazalisha mbolea yenye virutubisho vinavyotakiwa mwilini.

Alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi na madhara yaliyoletwa na vita vya Russia na Ukraine watahakikisha upatikanaji wa mbole unaimarishwa ili kuwezesha upatikanaji wa chakula.





Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuja na Kushoka Tools inayojihusisha na uzalishaji wa mashine za kutengenezea nishati mbadala, akitoa elimu ya utengenezaji wa mkaa kwa kutumia taka mbalimbali kwa vijana, wakati wa mafunzo yaliyofadhiliwa na Taasisi ya Tulia Trust, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima Kyela kupewa miche 100,000 ya michikichi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya imesema inatarajia kuzalisha miche 100,000 ya michikichi ya kisasa na kuigawa kwa wakulima, lengo likiwa ni kuhamasisha zaidi uzalishaji wa zao hilo.

Aidha, halmashauri hiyo imesema inahamasisha uzalishaji wa zao hilo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kupikia ili kupunguza kiwango cha uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kyela, Katule Kingamkono aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo cha robo ya kwanza, ambapo alisema uzalishaji wa miche hiyo ni mwendelezo wa utaratibu wa halmashauri.

Alisema miche hiyo ambayo wanazalisha ni miche ya kisasa ambayo inafanya vizuri kuliko ile ya asili ambayo wakulima wengi wamezoea kuitumia.

Kingamkono alisema katika mwaka wa fedha uliopita halmashauri hiyo ilizalisha zaidi ya miche 36,000 ya zao hilo na kuigawa bure kwa wakulima zaidi ya 900 ambao wamepanda na hivyo akasisitiza kuwa wataendelea. "Hii miche tunaigawa bure kwa wananchi baada ya kuizalisha ili kuwahamasisha wananchi wetu kuongeza uzalishaji, kilimo cha zao hili ni muhimu kwa sababu tunahitaji kuongeza uzalishaji wa mafuta nchini," alisema Kingamkono.

Alisema mbali na kuongeza uzalishaji wa mafuta nchini pia halmashauri hiyo inalenga kuongeza kiwango cha mapato yatokanayo na michikichi kwa maelezo kuwa itakuwa inapata ushuru kutokana na mauzo ya mafuta hayo.

Hata hivyo alisema kupitia kilimo hicho pia wataongeza kipato kwa mkulima mmoja mmoja wa wilaya hiyo hasa wale ambao wanashughulika na kilimo cha zao hilo. Vilevile alisema halmashauri hiyo inaendelea kuhamasisha wananchi kuzalisha mazao mengine yakiwemo ya chakula na biashara ili kuwa na uhakika wa chakula na kipato.

Baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo walishauri maofisa kilimo kuendelea kutoa elimu ya kilimo bora cha mazao mbalimbali ndani ya wilaya hiyo ili kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Mmoja wa madiwani hao, Mwaipetania Afundisye ambaye ni Diwani wa Kata ya Ipinda alisema ili kuhakikisha uzalishaji wa zao la michikichi linakuwa na tija, maofisa kilimo wanatakiwa kushiriki kwenye kila hatua ya uzalishaji.

Alisema msimu wa kupanda unapoanza maofisa hao wanatakiwa wawe wanashiriki kuanzia mwanzo wa uzalishaji wa miche, kupanda, kupalilia na kutoa elimu kuhusu huduma zingine zinazohitajika.

"Zao hili ni muhimu sana kwa wakulima wetu, ni vizuri maofisa kilimo wetu wakaanzisha mashamba darasa katika kila kata inayozalisha zao hili ili wakulima wawe wanajifunza zaidi," alisema Afundisye.

Diwani wa Kata ya Njisi, Omary Mwinjuma aliomba serikali kuwahisha mbolea ya ruzuku kwa wakulima ili kuwasaidia wakulima kuendana na msimu wa kilimo tofauti na ambavyo imekuwa ikitokea katika miaka ya nyuma.

Alisema wakulima wanapocheleweshewa mbolea wanashindwa kuendana na msimu na hivyo tija kwenye uzalishaji kupungua jambo ambalo alisema linarudisha nyuma juhudi za wakulima.

# Bajeti kusaidia malezi, makuzi ya mtoto kutengwa mwakani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema inakusudia kutenga bajeti maalumu katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM).

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya anayeshughulikia bajeti, Juma Maduhu aliyasema hayo kwenye kikao cha tathmini ya programu hiyo kilichofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kikishirikisha wadau mbalimbali.

Baadhi ya wadau walioshiriki kwenye kikao hicho ni pamoja na maofisa maendeleo ya jamii na maofisa ustawi wa jamii kutoka katika halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya pamoja na wadau kutoka katika taasisi binafsi.

Maduhu alisema alimshirikisha Katibu Tawala wa Mkoa huo kuhusu kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali za programu hiyo akakubali na hivyo wanasubiri muda ufike.

"Mimi mwenyewe nipo kwenye eneo la bajeti, kwahiyo hiki ninachokisema hapa ninakifahamu vizuri na tutahakikisha mwaka wa fedha ujao tunatenga bajeti ambayo itatosha kutekeleza hizi afua muhimu," alisema Maduhu.

Alisema endapo watafanikisha jambo hilo kama walivyopanga kuna uwezekano Mkoa wa Mbeya ukawa miongoni mwa mikoa ambayo itatekeleza kwa ufanisi zaidi.

Aliwataka wadau mbalimbali zikiwemo taasisi zisizokuwa za kiserikali kushiriki pia kwenye utekelezaji wa afua hizo ikiwemo masuala ya lishe kwa watoto pamoja na vitu vingine muhimu.

Mwakilishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Joel Mwakapala alishauri wadau wote wanaoshiriki kwenye utekelezaji wa programu hiyo kuhakikisha wanaifahamu vizuri ili waitekeleze kwa ufanisi.

Alisema wadau hao pia wanatakiwa kushiriki kutoa elimu kwa jamii kuhusu afua mbalimbali zilizomo kwenye programu hiyo na kuhakikisha inatekelezwa vizuri.

Aliwapongeza viongozi wa Mkoa wa Mbeya kwa kuendelea kubuni njia mbalimbali za kuitekeleza programu hiyo na akawataka waendelee kushirikiana katika kubuni na kutekeleza.

Nao baadhi ya washiriki waliahidi kwenda kuifanyia kazi kwenye maeneo yao kwa maelezo kuwa programu hiyo inalenga kuwasaidia watoto kukua katika misingi bora.

# Wakazi Njombe waiangukia serikali uhaba petroli, dizeli

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI wa Mkoa wa Njombe wameiomba serikali kuchukua hatua za haraka kutatua tatizo la uhaba wa mafuta ya dizeli na petroli, ambao unasababisha pia kupanda kwa bei za nauli.

Uhaba wa nishati hizo umefikia siku ya tatu sasa Mkoani Njombe, kwamba vituo viwili hadi vitatu vimekuwa vikitoa huduma ya mafuta, vingine vikikosa na kusababisha wanunuzi kutafuta mkoa mzima bila mafanikio.

Wakizungumza na Nipashe wananchi hao wamesema bei za usafiri wa bajaji nauli imeongezeka kutoka Sh. 500 hadi Sh. 1,000, usafiri wa pikipiki umepanda kutoka Sh. 1,000 hadi Sh.2,000 huku nauli za wilayani nazo zikipanda hadi Sh. 7,000 na Sh. 8,000 kutoka Sh.2,000 hadi Sh.3,000.

"Kwa hali hii tunaomba kama ni biashara ya mafuta ishuke bei, kutoka kijijini kufika hapa mjini imekuwa ni hasara tupu, ukiuliza tatizo ni nini unaambiwa ni mafuta" alisema Jonas Mgaya.

Kwa upande wao baadhi ya madereva wa vyombo vya moto akiwemo, Erasto Sanga alisema wameamua kupandisha bei hizo ili kwenda sawa na kupanda kwa bei ya mafuta wanayoyapata kutoka kwa walanguzi kwa bei ya Sh. 6,000 na Sh.7,000 baada ya kukosekana katika vituo vya mafuta.

"Hata kama mafuta yamepanda lakini sasa hayapo, baada ya hapo raia wanafuata mafuta mtaani, vijijini wakija wanatuuzia Sh.7,000, Sh.8,000 kwa hiyo inatokea kwamba abiria nitakaembeba hawezi kwenda na Sh.1,000 tena, unakwenda kuchukua lita tano unaambiwa shilingi 35,000 muda huo tungeenda pale ni Sh.17,000 mpaka hiyo fedha irudi ni saa ngapi" alisema Sanga.

Dereva mwingine, Michael Kihaka alisema serikali itafute namna bora ya kutatua changamoto ya mafuta kwa sababu siyo mara ya kwanza kutokea kwa changamoto kama hiyo.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Njombe, Boniface Kamoga alisema katika kipindi hiki mamlaka haijapandisha nauli na badala yake wanaendelea kuwafuatilia waliopandisha nauli na watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema: "Kwanza sisi hatujapata taarifa ya kupanda kwa nauli, nauli ni zile zile kwa upande wa bajaji na bodaboda hatuhusiki upande wa nauli kwa sababu ni vyombo vya kukodisha na bei anapanga kati ya abiria na dereva".



# CUF waomba marekebisho Sheria ya Uchaguzi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Wananchi CUF kimeitaka Serikali ya Zanzibar kupeleka muswada wa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi ili chaguzi zijazo kuwa huru na haki.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho, Hamad Masoud wakati akizungumza na waandishi wa Habari.

Hamad alisema CUF inataka katika mapendekezo hayo, kuondolewe uchaguzi wa kura ya mapema ambayo hupigwa na watu mamaalum ikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama siku moja kabla ya uchaguzi mkuu wa Zanzibar.

Alisema wanapendekeza kuwa uchaguzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar na uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa siku moja kwa watu wote na kila tume kusimamia uchaguzi wake.

Hamad alisema hakuna haja ya kuwa na kura ya mapema kwa sababu walengwa wa kura ya mapema hupiga tena kura kwa siku ya uchaguzi mkuu kwa ajili ya kumchagaua Rais wa Tanzania na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumzia kuhusu muundo wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar ambapo hivi karibuni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliteuwa na kuwaapisha wajumbe wa tume hiyo pamoja na mwenyekiti wake, alisema licha ya CUF kutoshirikishwa katika muundo huo lakini wao wanaiunga mkono tume hiyo.

Alisema kuwa imani yao wajumbe wa tume hiyo ni wanauzoefu mzuri kwasababu baadhi ya wajumbe ni wazoefu wa muda mkubwa wa chaguzi za Zanzibar.

Alisema CUF ni waumini wa falsafa ya Rais Samia ya maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na ujenzi mpya, hivyo CUF haioni haja ya kuendeleza majabizano na wanaunga mkono tume hiyo.

Pia alisema imani yao wajumbe wa tume hiyo akiwemo mwenyekiti wake watavaa viatu walivyopewa na kuivusha Zanzibar katika uchaguzi huru na haki.

Alisema hawana mashaka na utendaji wa wajumbe wa tume hiyo, lakini masikitiko yao ni kwamba CUF haijashirikishwa katika tume hiyo.

Alisema kwa mujibu wa kifungu hicho kwa kuzingatia takwimu za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar baraza la sasa halina kambi rasmi ya upinzani.

"Kwa mujibu wa sheria hii ilikuwa vyama vya siasa tuhusishwe katika mapendekezo ya uteuzi wa wajumbe wa tume hiyo, lakini CUF haina kumbukumbu yoyote ya kuhusishwa katika hatua hii muhimu ya tume ya uchaguzi" alisema.

Alisema wakati wa kipindi cha DK. Ali Mohamed Shein katika kutekeleza hizo aliviita vyama zote vya siasa Ikulu ili kushauriana katika kupatikana wajumbe wa tume ya uchaguzi.



Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, akizungumza katika mkutano wa kusikiliza kero za wananchi wa kijiji cha Bubwini Makoba, mkoani humo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Kongamano la TEHAMA ni muhimu katika ukuaji dijitali'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk Khalid Salum Mohamed, amesema kongamano la kuunganisha wadau wa TEHEMA na miundombinu lina mchango mkubwa katika ukuaji wa ulimwengu wa kidijitali.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano hilo na kusema kuwa dunia hivi sasa imebadilika, kwamba kumekuwa na mageuzi makubwa ya teknolojia ya kidijitali ambayo imerahisisha shughuli za binadamu.

Alisema katika kuhakikisha Tanzania inaimarika katika ulimwengu wa kidijitali Serikali ya SMZ na SMT zimekuwa zikifanya kazi kubwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Aidha, alisema minara 45 imeshawekwa kwa kushirikiana na Tigo-Zantel, Helios Towers , TTCL na UCSAF na kazi ya kuweka minara mingine inaendelea.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Uendeshaji wa Mitambo ya Mawasiliano ya Kampuni ya Tigo-zantel, Amos Bwire, alisema wameamuwa kushiriki kongamano hilo ili kupata fursa ya kusikiliza baadhi ya changamoto zinazowapata wateja wao, kupata njia za kuelekea kwenye suluhisho la kuzitatua changamoto hizo.

Aidha, alisema kuwa Tigo-zantel imeanza na mkakati wake mkubwa wa kuboresha huduma zao za mawasiliano kwenye maeneo yaliyokuwa na huduma ya 2G na 3G ambapo maeneo hayo yanaenda kupata huduma ya 4G.

# Utafiti wa magonjwa yasiyoambukiza kuanza kesho

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar inatarajia kufanya utafiti maalum wa kitaifa wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza ifikapo Septemba 9 mwaka huu.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh, alisema, utafiti huo utagusa kaya 540 ambazo kwa kutumia miongozo ya kitaalamu ya kiutafiti ndizo zilizobahatika kuchaguliwa na kuwemo katika utafiti huo.

Alisema kwa upande wa Pemba jumla ya kaya 180 na Unguja ni kaya 360 zitafikiwa na kuhojiwa.

Hata hivyo, alisema kuwa viongozi wakuu wa nchi wanaendelea kuchukua hatua thabiti za kuwekeza zaidi katika sekta ya afya kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Aidha, alisema hali ya magonjwa yasiyoambukiza imeendelea kuwa tishio kwa ustawi wa wanadamu duniani kote, kwamba kwa Zanzibar hali ya magonjwa haya pia imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Alisema lengo la utafiti huo ni kutathmini hali ya afya kuhusiana na viashiria hatarishi na mwenendo wa magonjwa yasioambukiza nchini, ambapo alisema kuwa utafiti kama huo ulifanyika mwaka 2011 Zanzibar na 2012 ulifanyika Tanzania Bara.

Alisema matokeo ya utafiti huo kwa Tanzania Bara hayakuwa mazuri, ambapo vihatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza vilibainisha kuwa hali ya ugonjwa wa kisukari ilifikia asilimia 3.7 na ugonjwa wa shinikizo la juu la damu ilikuwa asilimia 33.

Alisema viashiria hatarishi kama uzito uliokithiri ulifikia asilimia 14.3, na idadi ya watu wanaotumia sigara ndani ya kipindi cha utafiti ilikuwa asilimia 7.3, wanaotumia pombe asilimia 1.7 na watu ambao walikuwa wanajihusisha na mazoezi na kujishughulisha kwa kiwango kidogo kuliko inavyopaswa walikuwa asilimia 17.6.

Alisema utafiti ulionesha kwamba asilimia 97.9 ya watu walikuwa hawali mboga na matunda kwa kiwango stahiki.

Aidha, alisema hatua hiyo ni sehemu ya mpango wa wizara katika kuimarisha huduma za afya hasa ukizingatia kuwa maradhi yasiyoambukiza yakiwemo kisukari, shinikizo la damu, saratani, kinywa na meno yamekuwa yakiongoza kwa idadi ya vifo.

Naye, Meneja Kitengo cha Maradhi yasiyoambukiza, Dk. Omar Mohamed Suleiman, alisema, zoezi hilo litafanyika kitaalamu ambapo miongoni mwa masuala yatakayoulizwa ni hali ya matumizi ya vyakula pamoja na vinywaji.

Hivyo, aliwaomba wananchi kuendelea kushirikiana na Wizara ya Afya ili kuona magonjwa hayo yanatokomea.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JOACHIM ISDORI KIMATI** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 154045** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/8939/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEORGE V EDWARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1434/0063** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **PIUS SECONDARY SCEONDARY SCHOOL** mwaka 2008. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **MBL/RB/6778/2015**

## UPOTEVU WA VYOMBO VYA MOTO

**JOHNSON WILFRED MTEI** mwenye **TIN 116-735-261** anatangaza kupotea kwa vyombo vya moto alivyowahi kumiliki vyenye usajili namba: **T 721 CUL, MC 377 CHH, MC 808 CHA, MC 104 CGE, MC 290 AGU, MC 663 AGL na MC 529 ASV.**
POLISI TAARIFA:
**DAR/BUG/RB/254674/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ERICK RICHARD SAGALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T318DCK** aina ya VEROSA, Chassis No. **GX110-6035432.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/119875/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 57/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SAFINA JAPHET MRINDOKO wa AZINA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA JAPHET JEREMIA MRINDOKO**

## TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo Tarehe 06 Mwezi 09 Mwaka 2023.**

COURT SEAL DODOMA DISTRICT

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO-MJINI
DODOMA

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 90 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late ZEBEDAYO PAULO MLOHA of Michese within Dodoma city**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by JUMA ZEBEDAYO PAULO**

## GENERAL CITATION

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of 09,2023

Dated at Dodoma this 06 day of 09, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA / KIMATAIFA

# LATRA, EWURA waonya wasafirishaji kupandisha nauli

**Na Benny Kingson,** TABORA

BAADA ya bei ya mafuta kutangazwa kuongezeka kwa senti 16 kwa kila lita, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) na Baraza la Ushauri la Watumiaji Nishati ya Maji na Mafuta (EWURA CCC), mkoani Tabora zimewaonya wasafirishaji wa abiria kutotumia mwanya huo kutoza nauli kubwa kwa kisingizio cha mafuta kupanda bei.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA mkoani Tabora, Nelson Mmari, akiongea na gazeti hili ofisini kwake, alisema kuwa EWURA makao makuu wametangaza ongezeko hilo la bei ya mafuta, lakini hawajatangaza ongezeko la nauli.

Alisema wao ndio wenye mamlaka ya kutangaza ongezeko hilo na mara ya mwisho LATRA kutangaza ongezeko la nauli ilikuwa mwaka 2013 – 2022 na kuonya atakayebainika atachukuliwa hatua kali kisheria.

"Wasafiri wote watoe taarifa LATRA kupitia namba ya bure 0800110019 kama wataona nauli wamepandishiwa, wamekatiwa tiketi za kawaida badala ya za mtandaoni kwa mabasi yaendayo mikoani ama wakiona changamoto yoyote wawapo kwenye vyombo vya usafiri ili tuchukue hatua haraka," alisema.

Aliwatahadharisha wamiliki wa vyombo na wasafirishaji kutochukua hatua binafsi kwa kupandisha nauli kwa madai ni biashara huria na kwamba wanaenda na hali halisi ya gharama za mafuta na uendeshaji kwa kuwa wakibainika watachukuliwa hatua kali kisheria na kudhibitiwa ipasavyo.

Mmari aliwataka wamiliki na wasafirishaji hao kuhakikisha wanatumia tiketi mtandao kuwapatia abiria wao na endapo watabainika wamewapa tiketi za kawaida watatozwa Sh. 250,000 na kwamba wanaendelea kufanya msako wa kushtukiza kila wakati katika njia zote.

Alisema wanaendelea kuwasisitiza abiria kukata tiketi mtandao katika maeneo yanayotambulika na kuacha kuwapa pesa mpiga debe waliojaa vituoni ili kukwepa kuibiwa pia wanatafuta dawa ya kuwadhibiti wapigadebe hao wapatao 1,200 wanaoleta kero kwa abiria mjini humo.

Alisema kuna magari 150 ambayo yanafanya safari kwenda mikoani kila siku kutoka mkoani humo na wapiga debe hao ni tatizo kwa abiri na kwa watu wote waliopo kwenye kituo cha mabasi na kuahidi kuwashughulikia.

Ofisa Msaidizi huduma kwa wateja na utawala EWURA CCC Mkoa wa Tabora, Sakina Yusufu, aliwahimiza wadau na wananchi kuwa na tabia ya kupata taarifa sahihi kuhusu gharama halali za tozo ya maji na mafuta kutoka katika baraza hilo.

Sakina alisema, wadau na wananchi wanapaswa kutoa changamoto zao zinazowakabili katika mamlaka husika kama kupanda kwa nauli au bei za maji pasipokuwa na mpangalio ama taarifa toka mamlaka husika ili hatua za haraka zichukuliwe na kutatuliwa.

"Wadau na wananchi hususani wasafiri watambue kuwa ongezeko la bei ya mafuta lililotangazwa na serikali kupitia EWURA hakutoi mwanya wa nauli kupandishwa ama ruhusa ya kupandisha, ni kosa kisheria hivyo watoe taarifa kwetu kupitia namba 0746478361 ili tuchukue hatua haraka," alisisitiza.

Alisema wataendelea kutoa elimu zaidi kwa jamii kuhusu umuhimu wa kujua haki zao hasa bei za bidhaa maji na mafuta na kupata ufahamu wa masula muhimu mabalimbali ili kuondoa changamoto zilizopo na kazi iendelee.

Uchunguzi umebaini nauli wanazotozwa abiria kutoka na kwenda Wilaya ya Urambo ni Sh. 6,000 badala ya Sh. 5,000, Wilaya ya Nzega ni Sh. 6,000 - 7,000 badala ya Sh. 5,000, Wilaya ya Sikonge Sh. 5,000 badala ya Sh. 3,500-4,000 na 'bajaji' ni Sh. 1,500-2,000 badala ya kati ya Sh. 500- 1,000 'bodaboda' Sh. 1,500-2,000 badala ya Sh.1,000.

# Waziri Mkuu ataka ufumbuzi wa tembo kusumbua wananchi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema tatizo la wanyamapori kutoka hifadhini na kwenda kwenye makazi ya watu, linatafutiwa ufumbuzi na tayari kamati ya kukagua kubaini suala hilo imeshaundwa.

Majaliwa aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa akijibu swali la Mbunge wa Mwanga, Joseph Tadayo, wakati wa maswali ya papo kwa papo.

"Nchi yetu imetunga sheria nyingi nzuri za kulinda uhifadhi nchini na kuzuia uwindaji haramu kwa ajili ya kukuza utalii, ikolojia na kuongeza mapato ya taifa. Lakini hivi karibuni wanyamapori hao ambao wamehifadhiwa kwa kuzingatia sheria na mikataba ya kimataifa, wamegeuka kuwa janga kwa kuharibu mali za watu, kuvuruga miundombinu na hata kusababisha vifo vya watu wengi," alisema.

Mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mkakati gani kuhakikisha inapitia upya sheria hizo ambazo waliziweka kulinda uhifadhi ili pia ziwalinde wananchi na hata ikibidi kujitoa kwenye baadhi ya mikataba ya kimataifa ambayo inawashurutisha kuweka sheria za namna hiyo ambazo zinadhuru wananchi na mali zao.

Akijibu swali hilo, Waziri Mkuu alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, tayari jitihada zimechukuliwa ikiwamo wizara (ya maliasili na Utalii) kuunda kamati ya kukagua kubaini tatizo haswa la kusababisha wanyama kuingia kwenye makazi.

"Kamati ikikamilisha kazi, tutapata majibu, hivyo nimwombe mbunge ilimradi wizara ilishaanza kuweka timu ya kukagua na kugundua tatizo, kama itabainika na kuturudisha kwenye sheria, basi wizara itatuongoza kwa kuleta sheria hapa kwa mabadiliko ili kuhifadhi.

"Lakini pia tuhakikishe wananchi wanaendesha shughuli zao na maisha yao yanaimarishwa kama ambavyo tuliweka sheria hizi ziwalinde hapo mwanzo," alisema.

Majaliwa alisema ushauri wa mbunge huyo kwa serikali, umechukuliwa lakini kwa vile wameona wizara imeshaunda kamati, aliomba waiache ilete matokeo yake.

Majaliwa alisema serikali inajua ziko sheria zinalinda haya na mbunge ametaka wabadilishe lakini muhimu wanataka wizara ihakikishe maeneo yote yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kuweka wanyama yanaendelea kusimamiwa na sheria na taratibu ambazo wamezipanga kwa ajili ya kudhibiti wanyama hao kuingia kwenye makazi.

Alisema hiyo ni pamoja na kulinda bufa ambapo walitenga kilometa tano toka makazi kuingia kwenye msitu na baadaye wakaruhusu wananchi wafanye shughuli zao za uzalishaji mali kwenye eneo hilo la kilometa tano lakini sasa imeonekana wanyama wanavuka na kuingia kwenye makazi.

Majaliwa alisema kupitia vikao vya Bunge baadhi wabunge wamekuwa wakieleza usumbufu ambao wananchi wanaupata kwa wanyama waliohifadhiwa kwenye hifadhi kuvamia makazi ya watu na kuharibu mali na hata kusababisha vifo.

Alisema wamepata taarifa hizo mara nyingi kwenye miji iliyo kandokando na hifadhi ni kweli wanazo sheria zinazosimamia utekelezaji wa kuhakikisha wanyama wanabaki porini na wananchi wanaendesha maisha yao kwenye maeneo rasmi.

"Lakini pia, kumekuwa na wimbi la ongezeko la wanyama kwenye misitu yetu kutokana na jitihada za serikali kupitia sheria zetu hizo za udhibiti wa uhifadhi na kulinda uwindaji haramu. Hata hivyo, Wizara ya Maliasili imekuwa ikifanya taratibu kadhaa kukutana na taasisi zinazohusika kwenye uhifadhi wa mazingira yetu na hifadhi za wanyama wetu kuona wanyama wanabaki hifadhini.

"Baadhi ya jitihada zilizochukuliwa ni kuongeza idadi ya askari walioweka vituo kandokando ya hifadhi hizo kuzuia wanyama wasiingie kwenye makazi ya wananchi lakini pia jitihada za kufukuza wanyama kwa kutumia ndege kuwarudisha hifadhini," alisema.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (kulia), akizungumza na ujumbe wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), jijini Dodoma jana. Kushoto ni Rais wa TLS, Wakili Harold Sungusia. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Marekani kuipatia Ukraine mizinga yenye Uraniam

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imetangaza kuwa itasambaza makombora ya mizinga ya urani yaliyorutubishwa kwa ajili ya Ukraine kama sehemu ya msaada wa kijeshi wenye thamani ya bilioni moja.

Hatia hiyo imelaaniwa na Russia na kueleza kwamba mizinga hiyo ya Abrams na silaha zenye utata hazitavumika.

Tangazo hilo lilitolewa jana huku Ukraine ikiishutumu Russia kwa kuwaua watu 17 katika shambulio la kombora eneo la sokoni. Mpango huo mpya wa msaada wa usalama kwa Ukraine ulitangazwa wakati Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken akifanya ziara nchini Ukraine.

Uranium iliyorutubishwa kwa kawaida inakuwa imeondolewa makali mengi, lakini sio kwa athari inayotokana na mionzi.

Wakati huo huo, mashambulizi yanayoshukiwa kuwa ya ndege zisizo na rubani za Ukraine yaliripotiwa kufanyika katika mji wa Russia wa Rostov-on-Don na karibu na Moscow.

Video ambayo haijathibitishwa ilionyesha kile kilichoonekana kuwa mlipuko katikati mwa Rostov ambapo kulingana na Gavana Vasily Golubev, mtu mmoja alijeruhiwa na magari kadhaa kuharibiwa.

Alisema ndege mbili zisizo na rubani zililenga mji huo ulioko kusini mwa Russia na zote mbili ziliangushwa.

Meya wa Moscow Sergei Sobyanin alisema ndege isiyo na rubani iliyokuwa ikilenga mji wa Ramenskoye pia imedunguliwa na hakuna uharibifu ulioripotiwa.

# ZIMAMOTO, NGOME KUFUNGUA PAZIA LA LIGI ZANZIBAR 2023/24

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MAAFANDE wa Zimamoto wanatarajia kuwavaa Ngome katika mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa Septemba 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mau A.

Bodi ya Ligi Zanzibar (ZLB), imesema maandalizi kuelekea msimu mpya wa mwaka 2023/2024 yamekamilika na ligi hiyo itashirikisha timu 16 kutoka Unguja na Pemba.

Ligi hiyo itaendelea tena Septemba 14, mwaka huu ambapo kwenye Uwanja wa Mau A, wakongwe Malindi FC watavaana na Kipanga wakati dimba la Mau B litashuhudia Kundemba ikiwakaribisha Jamhuri kutokea Pemba.

**Mechi nyingine siku hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Kishindeni kwa kuwakutanisha wenyeji Chipukizi dhidi ya Mlandege kutoka Unguja.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohamed Ali Hilali, alisema matarajio yake atauwanza vyema msimu huu na kwa mafanikio makubwa.

Hilali alisema timu yake imejiandaa kuhimili mikiki ya ligi hiyo ambayo siku zote huanza kwa kasi kwasababu kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri katika michezo ya mwanzoni ilikujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa.

"Msimu huu hatuoni sababu ya kutopata ubingwa, tumefanya usajili unaoendana na Ligi Kuu, tumefanya maandalizi ya mapema ikiwamo kuwaweka wachezaji kambini hapahapa Unguja, lakini pia nyota hao wanafanya vizuri mazoezini na hata katika michezo kadhaa ya kirafiki ambayo tumecheza," alisema kocha huyo.

Ligi Kuu Zanzibar msimu mpya zitashuka timu nne na kubakiza klabu 12 kwa ajili ya msimu wa mwaka 2024/2025.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo inadhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) pamoja na Azam Tv wenye haki ya kurusha matangazo ya televisheni hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.




Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja wa Kampuni ya Sportpesa, Godwin Mweteni (kushoto), akimkabidhi mshindi Geofrey Ngassa simu janja, kupitia promosheni ya Maokoto Deilee kushirikiana na mtandao wa Tigo kupitia huduma ya TigoPesa. **PICHA: SPORTPESA**

# *Michezo kukutanisha watoto*

**Na Mwandishi Wetu**

JOJOO Fun Park imeandaa tamasha maalum ambalo litakutanisha watoto kutoka sehemu mbalimbali za jiji la Dar es Salaam kushiriki katika michezo pamoja na kujifunza mambo mbalimbali.

Tamasha hilo lilipewa jina la 'Holiday Picnic' linafanyika Jumamosi Septemba 9 kwenye ukumbi wa Jojoo Park, Kimara Bonyokwa ambapo mbali na michezo hiyo pia watoto watapata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali ya afya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mratibu wa tamasha hilo, Dk Asha Mahita, alisema wazazi pia watapa fursa ya kujifunza namna ya kutambua kipaji cha mtoto. Alisema kutakuwa na madaktari wa watoto ambao watatoa elimu juu ya umuhimu wa kuangalia afya ya watoto na ushiriki wao katika michezo.

"Tumeandaa Holiday Picnic ili kuwapa watoto a b c za afya na fursa ya wazazi kujifunza mambo muhimu katika malezi huku wakizingatia umuhimu wa afya zao," alisema Dk Mahita

Alisema moja ya mambo ambayo wazazi wanajisahau juu ya watoto wao ni kutowapa nafasi ya kushiriki michezo lakini pia kushindwa kufuatilia taratibu za kuwapatia chanjo zinazohitajika kwa watoto kulingana na umri wao

"Chanjo ni mojawapo ya hatua bora zaidi za afya ya umma na kuokoa watoto wanaokadiriwa kuwa milioni mbili mpaka tatu kwa mwaka. Hata hivyo, katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, viwango vya watoto wanaohudhuria kliniki kupata chanjo kimepungua, kwenye tamasha hili tutawakumbusha wazazi juu ya haya yote," alisema Dk Mahita

Alisema michezo mbalimbali itakuwepo kwa watoto kuanzia umri wa miaka 4-15 ambao watashiriki kucheza mpira wa miguu, riadha, kuogelea, kuvuta kamba na mengineyo.

## Kado, Mwasapili watua Pamba FC

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinacho onyesha imedhamiria kupanda daraja, Pamba FC ya Mwanza imewasajili wachezaji wazoefu wakiwamo kipa, Shaaban Kado, Hassan Mwasapili, Peter Mwalyanzi na Haruna Chanongo ili kuitumikia timu hiyo katika Ligi ya Championship itakayoanza keshokutwa.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana imesema wameamua kusajili wachezaji wazoefu ili kuhakikisha msimu ujao wanapanda daraja baada ya kushindwa kufikia malengo kwenye misimu mitatu iliyopita.

Nyota wengine waliosajiliwa na Pamba ni Tariq Abeid kutoka Ruvu Shooting, Ismail Mtamba (Ndanda FC), Mbaraka Mikelo, Emmanuel Mahige (Azam FC), Isah Ngoa (Ihefu), Lazaro Joseph, Rolland Msonjo na Rashid Mchelenga, Mtanzania aliyekuwa akichezea Polisi ya Kenya.

Klabu hiyo pia imemtangaza Mbwana Makata ndiye atakayekiongoza kikosi hicho katika kupambana na hatimaye kufikia malengo.

Pamba itaanza msimu mpya ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Nyamagana Septemba 11, mwaka huu kwa kuwaalika Cosmopolitan FC kutoka Dar es Salaam ambayo imepanda daraja.



## Ladies Open 2023 kufanyika Arusha

**Na ShufaaLyimo**

MASHINDANO ya wazi ya gofu kwa wanawake (Ladies Open) yanatarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 15 hadi 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kili jijini, Arusha imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), Queen Siraki, alisema licha ya wahusika wakuu wa mashindano hayo ni wanawake, mwaka huu wametoa nafasi kwa wachezaji wanaume kushiriki.

"Kwa sasa tunajiandaa na shindano letu kubwa la Ladies Open, wachezaji wetu wanaendelea vyema na mazoezi kuhakikisha wanakwenda kuonyesha ushindani," alisema Siraki.

Kiongozi huyo alisema kwa sasa timu za wanawake zimekuwa zikifanya vizuri katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki na kulitangaza vyema jina la Tanzania.

Hata hivyo ameuomba uongozi wa klabu ya gofu Lugalo kutoa ruhusa kwa wachezaji wake ili kushiriki mashindano hayo kwa lengo la kuongeza ubora wa michuano.

## ZISIKUPITE

### AL-ITTIHAD NA SALAH

KLABU ya Al-Ittihad ya Saudi Arabia jana iliwasilisha dau la pauni milioni 200 kumnunua nyota wa Liverpool kutoka Misri Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, ikiwa ni siku ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji. (***Telegraph***)

### TERRY KUJIUNGA AL-SHABAB

MLINZI wa zamani wa England na Chelsea, John Terry mwenye umri wa miaka 42, yuko mbioni kujiunga na Al-Shabab FC ya Saudia kama kocha. (***Sun***)

### LLORIS NJE YA UWANJA

GOLIKIPA wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 36, huenda akasalia nje ya uwanja hadi Januari huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa akiwa hajaonesha nia ya kuondoka licha ya Spurs kupokea ofa kadhaa. (***Guardian***)

### DIER KWENDA SAUDIA

BEKI wa Tottenham Hotspur na England, Eric Dier amefanya mazungumzo na mwenyekiti Daniel Levy baada ya kutemwa na kocha Ange Postecoglou. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Saudi Arabia. (***Telegraph***)

### NUNEZ ALITAKIWA

LIVERPOOL ilijaribu kumsajili mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 24, badala ya Joao Felix kabla ya mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 23, kujiunga na Barcelona kutoka Atletico Madrid. (***Mundo Deportivo***)

***

### PALHINHA NA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inatazamia kuwasilisha ofa mpya kwa kiungo wa Fulham Mreno Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28 Januari. (***Standard***)

### GUNDOGAN ALIIPUUZA ARSENAL

NAHODHA wa zamani wa Manchester City, Ikay Gundogan mwenye umri wa miaka 32 amekiri kwamba alipuuza nia ya Arsenal na klabu zingine msimu huu kwa sababu ya kutaka kuichezea Barcelona ili kuitimiza "ndoto ya utotoni" ya kiungo huyo wa Ujerumani. (***Mirror***)

### COLWILL ALISHAWISHIKA

BEKI wa Chelsea, Levi Colwill mwenye umri wa miaka 20 amefichua kuwa mchezajimwenza wa zamani wa Brighton na nyota wa zamani wa Liverpool, Adam Lallana alimshawishi kusaini mkataba mpya na kusalia Stamford Bridge chini ya kocha Mauricio Pochettino. (***Mail***)

### GRIEZMANN KUMFUATA MESSI

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 32, yuko tayari kuondoka Atletico Madrid mwisho wa msimu huu na kujiunga na Lionel Messi katika Ligi Kuu ya Soka ya Marekani. (***Sport, via Mail***)

### MBAPPE HATASAINI

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kuachana na nyongeza ya bonasi ya pauni milioni 68.6 katika mkataba wake na Paris St-Germain, lakini amesisitiza kwamba hatasaini mkataba mpya. (***90min***)

### HAZARD KUSTAAFU

NYOTA wa zamani wa Real Madrid na Chelsea, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 32 amedokeza kwamba anakaribia kustaafu. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI, HALLAND KUCHUANA TUZO YA BALLON D'OR 2023

**Nyota hao wanaongoza kwenye orodha ya wachezaji wanaowania tuzo hiyo kwa mujibu wa...**

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi na Erling Haaland wanaongoza orodha ya wachezaji 30 wanaowania tuzo ya Ballon d'Or 2023 baada ya jarida la Soka la Ufaransa kutangaza walioteuliwa juzi.

Uteuzi wa Messi unakuja mwaka mmoja baada ya kuondolewa kwenye orodha hiyo. Iwapo atashinda Ballon d'Or kwa wanaume mwaka huu, itakuwa ni mara yake ya nane kushinda tuzo hiyo, wa pili kwa wingi wa tuzo hizo ni Cristiano Ronaldo mwenye tano.

**Februari, Messi pia alishinda tuzo ya Mchezaji Bora kwa Wanaume wa FIFA kwa mara ya pili.**

Ronaldo, ambaye sasa anaichezea Al Nassr ya Saudi Arabia, hajatajwa kwa mara ya kwanza tangu 2003.

Mshindi atatangazwa katika hafla itakayofanyika ukumbi wa Theatre du Chatelet mjini Paris mnamo Oktoba 30 mwaka huu.

Messi aliiongoza Argentina kushinda Kombe la Dunia Desemba mwaka 2022.

Katika ngazi ya klabu, Messi hakuwa na wakati mzuri kule Paris Saint-Germain huku timu hiyo ya Ufaransa ikitupwa nje ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya 16 bora kwa msimu wa pili mfululizo, ingawa alisaidia timu hiyo kubeba taji la 11 la Ligue 1.

Aliamua kujiunga na Inter Miami kwa uhamisho wa bure, ambapo ameshinda kombe la Ligi na kutinga fainali ya U.S. Open.

Wakati huo huo, Erling Haaland pia anaweza kutoa ushindani mkubwa zaidi kwa Messi kwa tuzo hiyo.

Mshambuliaji huyo wa Norway alifunga mabao 52 katika michezo 53 kwenye michuano yote huku Manchester City ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alivunja rekodi ya msimu mmoja ya ufungaji wa Ligi Kuu ya England kwa mabao 36 katika kampeni yake ya kwanza nchini England.

Mshambuliaji huyo pia alishinda tuzo kadhaa kutokana na uchezaji wake mzuri, zikiwemo Mchezaji Bora wa Mwaka wa PFA, Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya England na Mchezaji Bora wa Mwaka wa Chama cha Waandishi wa Soka.

Orodha kamili waliowania tuzo ya Ballon d'Or:

Andre Onana - Manchester United/Cameroon, Josko Gvardiol - Manchester City/Croatia, Karim Benzema - Al Ittihad/Ufaransa, Jamal Musiala - Bayern Munich/Ujerumani, Mohamed Salah - Liverpool/Misri, Jude Bellingham - Real Madrid/England, Bukayo Saka - Arsenal/England , Randal Kolo Muani - Paris Saint-Germain/Ufaransa, Kevin De Bruyne - Manchester City/Ubelgiji, Bernardo Silva - Manchester City/Ureno, Emiliano Martinez - Aston Villa/Argentina, Khvicha Kvaratskhelia - Napoli/Georgia

Ruben Dias - Manchester City/Ureno, Nicolo Barella - Inter Milan/Italia, Erling Haaland - Manchester City/Norway, Yassine Bounou - Al Hilal/Morocco, Martin Odegaard - Arsenal/Norway, Julian Alvarez - Manchester City/Argentina, Ilkay Gundogan - Barcelona/Ujerumani, Vinícius Júnior - Real Madrid/Brazil

Lionel Messi - Inter Miami/Argentina, Rodri - Manchester City/Hispania, Lautaro Martinez - Inter Milan/Argentina, Antoine Griezmann - Atletico Madrid/Ufaransa, Robert Lewandowski - Barcelona/Poland, Kylian Mbappe - Paris Saint-Germain/Ufaransa, Kim Minjae - Napoli/Korea Kusini, Victor Osimhen - Napoli/Nigeria, Luka Modric - Real Madrid/Croatia, Harry Kane - Bayern Munich/England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,151,10
MECHI KALI
GEORGIA
VERSUS
SPAIN
1 | 8.05
X | 4.61
2 | 1.39
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO: USHINDANI WANGU NA MESSI UMEBADILISHA HISTORIA



CRISTIANO Ronaldo amesema ushindani wake na Lionel Messi "umetoweka," na tayari "umebadilisha historia ya soka."

Wawili hao wametawala mchezo huo kwa zaidi ya muongo mmoja, wakishinda mataji 79 kwa pamoja na kuwa wachezaji wawili pekee waliofunga zaidi ya mabao 800 kila mmoja.

"Sioni mambo kama hayo, ushindani umekwisha," amesema Ronaldo katika mahojiano na ESPN.

"Ulikuwa mzuri, watazamaji walipenda. "Wanaompenda Cristiano Ronaldo sio lazima wamchukie Messi na kinyume chake, tumefanya vizuri, tumebadilisha historia ya soka. Tunaheshimika duniani kote, hilo ndilo jambo muhimu zaidi.

"Amefuata njia yake na mimi nimefuata yangu, bila kujali kucheza nje ya Ulaya. Kwa nilivyoona, amekuwa akifanya vizuri na mimi pia. Urithi unaendelea, lakini sioni ushindani kama huo.

"Tulishiriki jukwaa mara nyingi, ilikuwa miaka 15. Sisemi sisi ni marafiki, sijawahi kula naye chakula cha jioni, lakini sisi ni wafanyakazi wenzake kitaaluma na tunaheshimiana."

Mshindi wa Kombe la Dunia Messi alijiunga na Inter Miami CF Juni kama mchezaji huru baada ya misimu miwili katika klabu ya Paris Saint-Germain.

Nahodha wa Argentina Messi ndiye mchezaji wa soka aliyepambwa zaidi aliposhinda kombe lake la 44 baada ya kuisaidia Inter Miami kubeba Kombe la Ligi 2023 Agosti.

Ronaldo, wakati huo huo, alishinda taji lake la kwanza akiwa na Al-Nassr ya Saudi Pro League, klabu ambayo alijiunga nayo Januari kutoka Manchester United, aliponyanyua Kombe la Ligi ya mabingwa ya Kiarabu mwezi uliopita.

Nahodha huyo wa Ureno amekuwa mchezaji pekee kufunga mabao 850 katika historia kufuatia kufunga kwenye ushindi wa 5-1 Jumamosi dhidi ya Al Hazem.

"Ni alama ya kihistoria," aliongeza Ronaldo mwenye umri wa miaka 38.

"Kwangu ilikuwa ni fahari kwa idadi niliyopata, ambayo sikufikiri ningeweza kufikia.

"Lakini nataka zaidi. Wakati wa kucheza mchezo."

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or pia anajivunia kuwa mwanzilishi wa wachezaji wengine nyota waliojiunga na Saudi Pro League.

Mwanzoni mwa majira ya joto, Karim Benzema na N'Golo Kanté walijiunga na mabingwa watetezi wa Saudi Pro League Al Ittihad, mlinda mlango wa Senegal Édouard Mendy alisajiliwa Al Ahli, na nyota wa zamani wa Chelsea Kalidou Koulibaly alijiunga na Al Hilal.

Zaidi ya hayo, Marcelo Brozovic alihamia Al-Nassr ya Ronaldo, Roberto Firmino alikamilisha uhamisho wa bila malipo kwenda Al Ahli baada ya kuondoka Liverpool, na nyota wa Brazil Neymar akasajiliwa Al Hilal kufuatia uhamisho wa euro milioni 90 kutoka PSG.

# *Mbappe, PSG wafikia pazuri*

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe yuko tayari kuachana na bonasi kubwa katika mkataba wake wa Paris Saint-Germain, lakini ameweka wazi tena kwa klabu hiyo kwamba hatasaini mkataba mpya, kwa mujibu wa 90min.

Mbappe aliamua msimu huu wa joto kwamba hataongeza mkataba wake wa sasa hadi 2025. Sasa, yuko mbioni kuondoka mwishoni mwa msimu kwa uhamisho wa bure.

Uamuzi wa Mfaransa huyo ulighadhabishwa na PSG, hadi akatemwa kwenye kikosi cha kwanza huku klabu hiyo ikijaribu kumuuza.


PSG ilikubali ofa ya uhamisho wa rekodi ya dunia kutoka kwa Al Hilal yenye thamani ya euro milioni 300 - lakini alikataa na hakuzungumza na timu hiyo ya Saudi Pro League.

Msimamo wa Mbappe siku zote umekuwa kwamba alitaka kucheza msimu huu akiwa na PSG kabla ya kuondoka, lakini wababe hao wa Ufaransa wamesisitiza kuwa hawakutaka kumpoteza kwa uhamisho wa bure.

90min inaelewa kuwa Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi alimwambia Mbappe hatavaa jezi ya PSG tena wakati wa mazungumzo na mama yake na wakala, Fayza Lamari.

Inaeleweka kuwa PSG wameendelea kushinikiza Mbappe kusaini mkataba mpya, uwezekano wa kujumuisha kifungu cha kutolewa ambacho kitamruhusu kuondoka kwake baadaye kwa ada iliyowekwa.

Hata hivyo, duru zinadokeza kwamba Mbappe amekubali kuondoa bonasi ya euro milioni 80 ambayo anastahili kulipwa katika msimu huu.



## HABARI MICHEZO

04,636/-

# NBC, TFF WAZINDUA CHAPA MPYA 'NBC CHAMPIONSHIP'

**Na Saada Akida**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) wamezindua rasmi chapa mpya ya Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza) itakayofahamika kwa jina la Ligi ya NBC Championship sambamba na uzinduzi wa ligi hiyo itakayoanza kesho kwenye viwanja mbalimbali nchini.

Ujio wa chapa hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mkataba wa udhamini uliosainiwa hivi karibuni baina ya pande hizo mbili unaotoa fursa kwa benki hiyo kuendelea na udhamini wake katika Ligi Kuu Tanzania Bara 'NBC Premiere League' hadi msimu wa mwaka 2027 wenye thamani ya Sh. bilioni 32.56, ambao unajumuisha Ligi za Vijana za klabu zinazoshiriki Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza.

Tukio la uzinduzi wa chapa hiyo mpya limefanyika jana jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa mchezo huo wakiwamo viongozi waandamizi wa NBC na TFF.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Binafsi, Elibariki Masuke, alisema ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo kuendelea kuiboresha ligi hiyo kwa kuangazia misingi muhimu ikiwamo kukuza vipaji vya wachezaji na kuongeza ushindani katika mchezo huo uliofanikiwa kuteka hisia za mashabiki wengi hapa nchini.

"Ni wazi kwa sasa mchezo wa soka hususani ligi yetu imegeuka kuwa si tu kivutio cha burudani kwa mamilioni ya wapenda mchezo huu bali umekuwa ni jukwaa wezeshi la kijamii na kiuchumi, kwa kutoa fursa za ajira, kurahisisha shughuli za kiuchumi. Mafanikio haya yamekuwa muhimu sana kwetu sisi kama taasisi ya kifedha kwa kuwa yanatoa fursa kwetu kuhudumia kundi kubwa la wanamichezo na wadau wa sekta hii muhimu," alisema Masuke.

Naye Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa TFF, Boniface Wambura, ambaye alimwakilisha Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia, pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa jitihada zake za kuendelea na kuongeza udhamini wake katika mchezo huo alisema udhamini huo kwenye upande wa soka la vijana na Ligi ya NBC Cjampionship utaimarisha pia Ligi Kuu ya NBC kutokana na ongezeko la vipaji vitakavyokuwa na ushindani.

"Imekuwa ni bora zaidi kwetu kwa sababu hii ni mara ya kwanza kupata mdhamini mmoja anaweka nguvu kwenye ligi zetu. Umuhimu wa hatua hii unaonekana zaidi katika urahisishaji wa maamuzi muhimu bila uwapo wa miingiliano ambayo muda mwingine ingeweza kutuchelewesha. Tunawashukuru sana NBC kwa kuona umuhimu wa kuchukua mnyororo mzima wa hizi ligi ambazo kiukweli zinategemeana sana...hivyo tunatarajia mafanikio zaidi kwenye soka letu," alisema Wambura.

Aliongeza mafanikio hayo ni ushahidi wa imani ya wadau mbalimbali nchini katika mchezo huo na viongozi wake kwa ujumla.




Mkurugenzi wa Wateja wadogo na Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (wa tano kutoka kushoto) na Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa TFF, Boniface Wambura (wa sita kutoka kulia) wakijipongeza pamoja na wafanyakazi wa taasisi hizo baada ya kuzindua chapa mpya ya Ligi ya Championship ambayo sasa inafahamika kwa jina la NBC Championship. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taifa wavu kibaruani Misri

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya taifa ya mchezo wa wavu (Almasi Kings) inatarajiwa kushuka dimbani kuvaana na Rwanda katika mchezo wa raundi ya 16 bora utakaochezwa leo.

Akizungumza na gazeti hili kutoka Cairo, Misri jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alfred Selengia, alisema wachezaji wake wamejiandaa vyema kuelekea mchezo huo.

Selengia alisema ataingia katika mchezo huo kwa tahadhari kwa sababu anafahamu anakutana na timu yenye wachezaji wengi wazuri na wenye uzoefu.

"Malengo yangu ni kufuzu na kuingia hatua ya robo fainali, ninaomba Watanzania waendelee kutuombea dua ili turudi nyumbani tukiwa na matokeo mazuri," alisema Selengia.

Kocha huyo alisema kila mchezaji ana morali ya mchezo huo na kusema jana jioni walifanya mazoezi ya mwisho ambayo yalikuwa maalumu kuiweka miili yao sawa.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.09/09/23 | 17:00 | AFC Wimbledon vs Stockport County FC | 2.75 | 3.20 | 2.47 |
| 02.09/09/23 | 17:00 | Milton Keynes Dons vs Notts County | 2.60 | 3.55 | 2.41 |
| 03.09/09/23 | 17:00 | Accrington Stanley vs Mansfield Town | 2.95 | 3.40 | 2.24 |
| 04.09/09/23 | 17:00 | Crawley Town vs Newport County | 3.00 | 3.30 | 2.25 |
| 05.09/09/23 | 17:15 | Burgos CF vs SD Eibar | 2.80 | 2.90 | 2.65 |
| 06.09/09/23 | 19:30 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.25 | 2.90 | 3.40 |
| 07.09/09/23 | 20:45 | Cobh Ramblers vs Athlone Town AFC | 2.36 | 3.40 | 2.48 |
| 08.09/09/23 | 22:30 | Virgin Islands, British vs Turks and Caicos Islands | 2.44 | 3.30 | 2.45 |
| 09.10/09/23 | 00:00 | Cerro Largo FC vs CA Fenix Montevideo | 2.46 | 3.00 | 2.60 |
| 10.10/09/23 | 03:30 | FC Tulsa vs Phoenix Rising FC | 2.41 | 3.25 | 2.50 |
| 11.10/09/23 | 04:00 | Colorado Springs Switchbacks FC vs San Antonio FC | 2.60 | 3.25 | 2.34 |
| 12.10/09/23 | 05:30 | Portland Timbers vs Los Angeles FC | 2.65 | 3.50 | 2.19 |
| 13.10/09/23 | 14:30 | Shanghai Jiading City Dev vs Heilongjiang Ice City | 2.60 | 3.15 | 2.40 |
| 14.10/09/23 | 16:00 | Kazakhstan vs Northern Ireland | 2.55 | 2.90 | 2.60 |
| 15.10/09/23 | 16:00 | CA Cerro vs CA River Plate (URU) | 2.42 | 2.95 | 2.70 |
| 16.10/09/23 | 19:00 | Faroe Islands vs Moldova | 2.80 | 2.90 | 2.40 |
| 17.10/09/23 | 21:00 | Tristan Suarez vs Deportivo Riestra | 2.75 | 3.00 | 2.60 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 08/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1129 | Taiwan vs Philippines | 2.74 | 3.37 | 2.52 |
| 14:00 | 1407 | Hapoel Bueine vs SC Tira | 2.85 | 3.05 | 2.28 |
| 14:30 | 5204 | Singapore vs Tajikistan | 3.92 | 3.50 | 1.93 |
| 14:30 | 5289 | Hapoel Migdal Haemeq vs Ironi Nesher | 1.77 | 3.60 | 3.60 |
| 16:00 | 3756 | FC Kremin Kreminchuh vs FC Ingulets | 4.35 | 3.70 | 1.64 |
| 17:30 | 1025 | NK Bistrica vs NK Ilirija | 2.24 | 3.38 | 2.72 |
| 17:30 | 3353 | NK Sesvete vs NK Vukovar 91 | 2.97 | 3.18 | 2.18 |
| 17:30 | 3366 | OFK Vrsac vs Macva Sabac | 2.08 | 2.85 | 3.45 |
| 18:45 | 5353 | Saffle FF vs FBK Karlstad | 3.31 | 4.07 | 1.81 |
| 19:00 | 3059 | Sweden U21 vs Macedonia U21 | 1.22 | 5.28 | 11.17 |
| 19:00 | 4371 | SK Hranice vs Blansko | 2.30 | 3.72 | 2.52 |
| 19:00 | 4381 | Krka vs ND Gorica | 2.22 | 3.33 | 2.78 |
| 19:00 | 4577 | Tampere United vs Atlantis FC | 2.41 | 4.03 | 2.29 |
| 19:00 | 4793 | Georgia vs Spain | 8.05 | 4.61 | 1.39 |
| 19:15 | 3914 | Germany U21 vs Ukraine U21 | 1.59 | 3.77 | 4.89 |
| 19:30 | 1218 | Netherlands U21 vs Moldova U21 | 1.03 | 9.97 | 40.69 |
| 20:00 | 5914 | Bron Radom vs Concordia Elblag | 2.15 | 3.52 | 2.85 |
| 20:30 | 2121 | US Marignane vs Nancy | 2.88 | 3.14 | 2.38 |
| 20:30 | 2872 | Chojnice vs Skra Czestochowa | 2.23 | 3.31 | 2.85 |
| 20:30 | 3013 | Epinal vs Sochaux | 2.16 | 3.30 | 3.15 |
| 20:30 | 3530 | Dijon vs Villefranche Sur Saone | 1.83 | 3.56 | 3.87 |
| 20:30 | 4510 | FC Goal vs FC Martigues | 2.69 | 3.25 | 2.47 |
| 20:30 | 5385 | Niort vs Cholet | 2.29 | 3.30 | 2.89 |
| 20:30 | 5718 | Nimes vs Chateauroux | 2.15 | 3.25 | 3.20 |
| 21:00 | 1609 | Santiago Morning vs Puerto Montt | 2.06 | 3.15 | 3.35 |
| 21:00 | 4023 | Poland U21 vs Kosovo U21 | 1.20 | 5.48 | 12.17 |
| 21:30 | 1672 | Ruthin Town vs Bangor 1876 FC | 2.12 | 4.35 | 2.45 |
| 21:30 | 3310 | Abergavenny Town vs Cwmbran Celtic | 4.14 | 3.73 | 1.67 |
| 21:30 | 3829 | Afan Lido vs Briton Ferry | 4.24 | 3.93 | 1.61 |
| 21:30 | 4975 | Ireland U21 vs Turkey U21 | 2.00 | 3.21 | 3.47 |
| 21:30 | 5012 | Prestatyn Town vs Holywell Town | 4.23 | 3.88 | 1.62 |
| 21:30 | 5551 | Taffs Well vs Carmarthen Town AFC | 3.83 | 3.73 | 1.72 |
| 21:45 | 1000 | Turkey vs Armenia | 1.33 | 5.08 | 8.88 |
| 21:45 | 1533 | Cardiff Met Uni. vs Pontypridd Town | 1.76 | 3.53 | 3.89 |
| 21:45 | 1900 | Malta U21 vs Spain U21 | 45.79 | 9.97 | 1.02 |
| 21:45 | 2110 | Luxembourg vs Iceland | 2.65 | 3.19 | 2.71 |
| 21:45 | 2453 | Croatia vs Latvia | 1.16 | 6.69 | 19.86 |
| 21:45 | 4409 | Cyprus vs Scotland | 9.28 | 4.85 | 1.34 |
| 21:45 | 4840 | Bosnia and Herzegovina vs Liechtenstein | 1.08 | 10.12 | 31.64 |
| 21:45 | 5015 | Treaty United vs Wexford Youths | 2.40 | 3.43 | 2.48 |
| 21:45 | 5324 | Slovakia vs Portugal | 6.60 | 4.00 | 1.52 |
| 21:45 | 5454 | Bray Wanderers vs Galway United | 6.08 | 4.56 | 1.38 |
| 21:45 | 5939 | Kerry FC vs Longford Town | 4.65 | 3.95 | 1.56 |
| 22:00 | 1808 | Willem II Tilburg vs Maastricht | 1.39 | 4.70 | 6.13 |
| 22:00 | 1904 | Saudi Arabia vs Costa Rica | 2.25 | 3.39 | 3.13 |
| 22:00 | 1993 | Finn Harps vs Waterford Utd | 7.85 | 4.83 | 1.29 |
| 22:00 | 3251 | Sevilla FC W vs Tenerife Sur W | 2.03 | 3.35 | 3.25 |
| 22:00 | 5508 | Levante vs Espanyol | 2.34 | 3.07 | 2.97 |
| 23:00 | 2593 | Haiti vs Cuba | 1.54 | 3.71 | 5.48 |
| 23:00 | 4097 | Belize vs Saint Vincent and the Grenadines | 1.85 | 3.26 | 3.98 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Septemba 8, 2023

Nipashe


UK. 22




**Ronaldo: Ushindani wangu na Messi historia**




Kiungo wa Yanga, Salum Abubakary 'Sure Boy' (kushoto) akiwania mpira dhidi ya Jesus Moloko, katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea kwenye Uwanja wa Avic Town ulioko Kigamboni, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Gamondi awaita mashabiki Kigali

**Na Faustine Feliciane**

ZIKIWA zimebaki siku nane tu kabla ya mchezo wa kwanza wa hatua ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema litakuwa ni jambo kubwa na la muhimu endapo mashabiki watasafiri kwenda Kigali, Rwanda ili kuishangilia timu yao.

Yanga itacheza dhidi ya Al Merrikh ya Sudan kwenye Uwanja wa Pele nchini humo baada ya wapinzani wao kuuchagua kama uwanja wao wa nyumbani katika michuano hiyo mikubwa katika ngazi ya klabu barani Afrika.

Akizungumza na Nipashe, Gamondi, alisema kuna ugumu kucheza viwanja vya ugenini lakini kunapokuwa na wingi wa mashabiki wa timu yako kunawapa molari na hamasa wachezaji wake uwanjani.

Gamondi alisema timu yake imekuwa ikiendelea vyema na maandalizi na kila mchezaji anaonyesha ana kiu ya kupambana na hatimaye kufikia malengo ya klabu.

"Mashabiki wana nafasi kubwa sana katika mchezo, kwa maandalizi tunayoendelea kuyafanya na idadi kubwa ya mashabiki kama watakuja uwanjani itatupa hamasa kubwa na nina uhakika tutafanya vizuri," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema atahakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo kwa sababu tayari mikakati imekamilika kwa asilimia kubwa.

"Mipango inaenda vizuri kama benchi la ufundi tulivyopanga, siwezi kusema tutafanya nini siku ya mchezo lakini kitu kizuri nimewasoma wapinzani wetu na nimejua ubora na mapungufu yao yapo wapi, naamini utakuwa mchezo mzuri sana," alisema Gamondi.

Aliongeza amepata mikanda ya video ya mechi walizocheza hivi karibuni ambayo anaamini itamsadia kuwafahamu vyema wapinzani wao.

Baada ya mchezo huo utakaochezwa Septemba 16, mwaka huu huko Kigali, Yanga itawakaribisha Wasudan hao kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam katika mchezo wa marudiano utakaofanyika kati ya Septemba 28 na 30, mwaka huu.

Mshindi wa jumla wa mechi hizo mbili atafanikiwa kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka kwa kuandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

# SIMBA YAANIKA SIRI KURUNDIKA MAKIPA

## Lengo la Mnyama ni kufikia malengo katika mashindano...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ngao ya Jamii, Simba wamesema hawana shida yoyote kutokana na uamuzi wao wa kusajili idadi kubwa ya magolikipa kwa sababu imeandaa mikakati maalumu itakayohakikisha wachezaji hao wote wanatumika, imefahamika.

**Kwa sasa Wekundu wa Msimbazi ina makipa watano na idadi hiyo kubwa imetokana na mashindano mengi yanayowakabili, ikiamini wote watakaa langoni kuitumikia timu hiyo.**

Makipa hao ni pamoja na Aishi Manula, Ally Salim, Hussein Abel, Ayoub Lakred na Ahmed Feruzi, aliyepandishwa kutoka katika timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (U-20).

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamegundua moja kati ya sababu ambazo timu zote kubwa zinafanya vizuri kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa ni kuwa na makipa wengi ambao ni bora na waliokamilika.

"Siyo dhambi kuwa na makipa wengi, tunataka tuwe na machaguo mengi, pia msimu huu tuna mashindano mengi kwa hiyo ni lazima tuwe nao wengi tena bora, niwakumbushe tu makipa tulionao si wale wa bora liende ni makipa kweli...

Lakini tukaona twende Morocco kumchukua Ayoub Lakred, hii ni kuonyesha tumedhamiria kufanya vizuri na ukitaka kufanya vizuri ni lazima eneo la kipa lazima liwe zuri kwa asilimia 100, pia tuna kipa chipukizi, Ahmed Feruzi," alisema Ahmed.

Aliongeza usajili wa Lakred, raia wa Morocco ulitokana na Mbrazil, Luis Jefferson kuumia na Hussein alichukuliwa kwa ajili ya kuziba nafasi ya Beno Kakolanya.

"Hatujawasajili makipa wote hao kwa bahati mbaya kama watu wanavyodhani, kila aliyesajiliwa ilikuwa ni kwa sababu maalum na hakuna shida, ila tu kama hali itakwenda vinginevyo tunaweza kumtoa Feruzi, kipa wetu tuliyempandisha kutoka timu ya vijana chini ya miaka 20 kwa mkopo katika klabu nyingine ili aendelee kupata dakika nyingi za kucheza, ni kipa mzuri, tuna mipango naye ya muda mrefu, na kwa uwezo wake anaweza kuwa kipa namba moja katika timu yoyote ile ya Ligi Kuu hapa nchini," Ahmed alisema.

Kuhusu maandalizi ya mechi ya michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos, Ahmed alisema mazoezi yanakwenda vizuri na bado timu yao itaendelea kucheza michezo ya kirafiki.

"Hizi tulizocheza ni mechi mazoezi, lakini tutakuwa na mechi zenyewe za kirafiki, ukisikia mechi ya kirafiki ni ile ambayo mwalimu anatakiwa kuona ni jinsi gani vijana wake wamemwelewa na unatakiwa kucheza bila presha, kocha anataka aone ikiwa hakuna mashabiki lakini mchezaji anacheza kwa woga basi anahitaji mafunzo zaidi, ndiyo msingi wa mechi za kirafiki, sio kushindwa wala kupata ushindi," alisema meneja huyo.

Mashindano ambayo Simba inachuana msimu huu ni Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Mabingwa Afrika, African Football League, Kombe la FA na michuano ya Kombe la Mapinduzi itakayoanza mapema mwakani.

Katika mechi mbili za Ligi Kuu ilizocheza, Simba ilianza kwa ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya wenyeji Mtibwa Sugar na ilipata ushindi wa magoli 2-0 ilipowaalika Dodoma Jiji FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >